# MAIMAMU WA AHLUL BAIT UJUMBE NA JIHADI

أئمة أهل البيت رسالة وجهاد

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul- Karim Juma Nkusui

ترجمة

# أئمة أهل البيت رسالة وجهاد

تأ ليف

الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978 - 9987 –17 – 074 – 6

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul- Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Sheikh Hemedi Lubumba

**Kimepitiwa na:**
Mbaraka A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Octoba, 2014
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ........................................................... 1

Vijana wetu na Maimamu wa Ahlul Bayt (as) ................................ 5

Jukumu la Maimamu katika maisha ............................................... 9

Maimam ni utekelezaji wa misingi ................................................. 9

1. Thamani ya haki................................................................... 12

2. Thamani ya uvumilivu na kujitoa muhanga........................ 13

3. Thamani ya ikhilasi ............................................................. 14

Maimamu ni Viongozi wa Kisharia .............................................. 16

Maimamu na Jukumu la Ujumbe .................................................. 24

Kadhia ya kisharia........................................................................ 28

Hakuna kunyamazia dhulma......................................................... 31

Misingi ndio kipimo..................................................................... 32

Sifa Za Maimamu ........................................................................ 35

Umaasumu ni dharura ya uongo .................................................. 36

Uwezo wa kielimu ........................................................................ 43

a. Jambo la kielimu:................................................................ 46

b. Uchambuzi mzuri................................................................ 47

c. Kutangulia katika elimu ya sayansi .................................... 48

Ukamilifu katika kila kitu ........................................................ 52
Ushujaa na uvumilivu ............................................................... 53
Uvumilivu wa Husein ............................................................... 57
Mapambano ya Maimamu .......................................................... 58
Tabia njema ............................................................................... 60
Ibada katika kilele ...................................................................... 62
Maisha ya Maimamu.................................................................. 68

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *Aimmatu Ahlu 'l-Bayti Risalata wa Jihad,* kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar. Sisi tumekiita, *Maimamu wa Ahlul Bait Ujumbe na Jihadi.*

Mwandishi wa kitabu hiki anazungumzia kuhusu umuhimu wa Maimamu na uongozi wao katika Umma huu wa Waislamu. Hata hivyo, Maimamu hao lazima wawe waadilifu na maasumu; na Maimamu wenye sifa hizo hawapatikani popote ila kutoka Nyumba ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ambao wameteuliwa na yeye mwenyewe kwa amri ya Allah *'Azza wa Jalla.* Maimamu hawa wanajulikana kwa jina la "Maimamu wa Ahlul Bait " ambao ndio Maimamu (Viongozi) wa Umma huu wa Waislamu kwa mujibu wa maelekezo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe.

Hadithi sahihi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na suala hili utazikuta ndani ya kitabu hiki zilizosimuliwa na wanazuoni wote wa Kiislamu - Shia na Sunni.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini

yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa Kiswahili kutoka lugha ya asili ya Kiarabu. Aidha tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**MCHAPISHAJI**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

Sifa zote njema anastahiki Mola Mlezi wa viumbe. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie rehema na amani Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyomteremshia amani Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, na umbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, hakika Wewe ni mwenye kuhimidiwa Mtukufu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu**.

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ
مُسْتَطِيرًاوَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا
وَأَسِيرًا إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً
وَلَا شُكُورًا إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا
فَوَقَاهُمُ اللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّاهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا
وَجَزَاهُمْ بِمَا صَبَرُوا جَنَّةً وَحَرِيرًا

"Wanaotimiza nadhiri, na wanaoogopa siku ambayo shari yake inaenea. Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na mateka. Hakika tunawalisha kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu tu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika tunaogopa kutoka kwa Mola Wetu siku ya kukunja uso yenye giza kali. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha. Na atawalipa Bustani za hariri kwa vile walivyosubiri." (Suratul- Insaan: 7 – 12).

بسم الله الرحمن الرحيم

# VIJANA WETU NA MAIMAMU WA AHLULBAYT (AS)

Mtoto anayezaliwa katika mazingira ya kidini yenye kujihifadhi, anapofungua macho yake na kufungua masikio yake na kufahamu hisia zake, huona mengi kati ya mwonekano wa utukufu na wa mapenzi ya kuwapenda Ahlul-Bayt watukufu (as) kutoka kwa watu wake na jamii yake. Baba yake anapotaja jina la Imam Ali, au Imam Hasan au Imam mwingine yeyote, haraka mtoto hufuatiliza kwa maneno ya kumsalia na kumtukuza. Na mama yake anapokabiliwa na tatizo lolote au jambo gumu haraka hutawasali kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa mmoja wa Maimam kwa kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu kwa haki ya Husain, Ewe Mwenyezi Mungu kwa haki ya mdhamini wa pepo." n. k.

Na katika minasaba ya kumbukumbu za Maimam kama vile Muharam na Swafar, mtoto huona mabadiliko makubwa na mageuzi katika maisha ya ahali yake na mazingira yake ambapo jamii huishi katika ratiba maalumu katika siku za Ashura na katika siku za kumbukumbu ya vifo, na hivyo huhudhuria katika wakati wa maombolezo na huacha kazi katika baadhi ya siku, na mandhari ya furaha na raha hutoweka katika jamii, hakuna kuoa, wala sherehe, wala furaha katika siku za Muharam, na yanatawala kwa watu mandhari ya huzuni na unyonge, yote hayo kwa ajili ya Imam Husain na Maimam wengine.

Mtoto anaona mandhari haya na anaishi nayo, na kutengeneza katika nafsi yake hali ya kuwatukuza moja kwa moja Maimam am-

bao majina yao yanakaririwa katika masikio yake, na anashiriki katika kuhuisha maadhimisho yao na kumbukumbu zao pamoja na mzazi wake na jamii yake. Na hivyo yanapandwa katika moyo wake mapenzi ya kuwapenda Maimam na hali ya kuwaheshimu, bila ya kujua chochote kuhusu maisha ya Maimam hawa, au jukumu lao au wasifu wao ambao umewapa wao mazingatio yote haya na kutukuzwa huku.

Na mtoto anakua na kuleleka na anaingia Madrasa na anaanza msafara mrefu wa kujifunza, akipita hatua za masomo, hatua kwa hatua, darasa kwa darasa, na anajifunza elimu na maarifa mbalimbali kisha anakutana na vyombo vya habari na maarifa vilivyopo katika jamii, radio, runinga na magazeti, na anajua kupitia masomo yake na maarifa yake shakhisiya za kihistoria na watu mashuhuri na anasoma majukumu yao na huduma yao, ambayo waliitoa kwa ubinadamu na wakastahiki kwayo utukufu na heshima. Na haraka linajitokeza kwake swali pana linalosema: Iko wapi nafasi ya Maimam katika historia? Liko wapi jukumu lao katika maisha? Yako wapi mafanikio yao katika medani ya elimu?

Amesoma historia katika shule na hajaona nafasi ya Maimamu katika viti vya ukhalifa au viti vya utawala. Makhalifa ambao historia imezungumzia juu yao ni wa: Bani Ummaya, Bani Abbasi na Uthmainiyyah! Na amekwishasoma historia ya upanuzi wa dola ya Kiislamu na akajua mashujaa mashuhuri wa upanuzi huo ni watu kama vile Khalid bin al-Walid, al-Muthanaa bin Harithah, Sa'ad bin Abiy Waqaasi, Twariq bin Ziyaad, Musa bin Naswir, Swalahu Diyn al- Ayubiy, lakini hajaona nafasi ya Maimam katika uongozi wa jeshi au mchango wao katika vita vya upanuzi !

Na anasoma kitabu cha sayansi hakuti majina ya Maimamu katika orodha ya maulamaa na wavumbuzi na wagunduzi pembezoni mwa jina la: Bastoor mvumbuzi wa darubini, Adson mvumbuzi

wa umeme, Is'haaq Newton mvumbuzi wa nguvu ya mvutano na wengineo! Na anajiuliza: Hivi kwa nini tunawatukuza Maimamu? Kwa nini kuwe na mazingatio yote haya makubwa ambayo wanayaonyesha watu wangu na jamii yangu kwa Maimamu! Ni jambo linaloingia akilini kumtukuza mmoja wa Makhalifa kwa sababu ya kubeba jukumu la uongozi wa umma na kukesha kwa ajili ya maslahi yake kwa muda mrefu, na kumjali mmoja kati ya wapanuzi wa dola kwa sababu alipanua dola ya Kiislam, na amechangia katika kueneza Uislamu, na kumtukuza mmoja wa wavumbuzi kwa sababu alitumikia ubinadamu kwa uvumbuzi wake.

Ama Maimamu kwa nini tunawatukuza na kuwaheshimu? Na wao si kingine isipokuwa ni kundi la wachamungu, walikuja kabla ya karne kumi na tatu na wakamaliza maisha yao kwa swala na dua kisha wakafariki dunia na mambo yakasonga mbele.

Ni katika wakati kama huu upepo wa shaka na upotovu huvuma mbele yake kwa sauti: Je haujawadia wakati wa kufahamu kutoendelea kwa watu wako na upotovu wa mila zao? Je, hujapata uhakika wa kudumaa kwao katika kuwatukuza watu wa kihistoria ambao hawakuwa na mchango wowote katika mambo yaliyopita wala athari yoyote katika mambo yaliyopo? Na unatokea mgongano mkali ndani ya nafsi ya kijana maskini baina ya malezi yake na masomo yake, baina ya mila zake na utamaduni wake, na inaingilia kati roho ya kukataa ambayo inaletwa na hatua ya ujana, na hivyo hukataa malezi yake na kuasi dhidi ya mila zake na hudharau nembo za dini yake.

Hakika watakasirika watu wake na wakuu wa jamii yake kwa tabia yake ya uasi, vitendo vyake vya dharau na watamhukumu kwa ukafiri wake na upotovu wake, wakati ambapo yeye ataendeleza mapambano yake na uasi wake. Na vivyo hivyo watatumbukia watoto wetu katika dimbwi la upotovu na kupotea vijana wetu katika jangwa la upotovu.

Na kama tutatafakari kwa makini katika jambo hili tutakuta kwamba msingi wa tatizo ni kutofahamu kijana huyu anayeinukia dhana ya dini yake, na kutokuelewa kwake historia yake na misingi yake, hakika yeye ameshuhudia wakati wa utoto wake nembo za kidini lakini hakujua maana yake, hakika ameona ganda tu na hakufahamu kiini na ameona gamba tu, na hakuona picha. Amewaona watu wake wanawatukuza Maimam bila ya yeye kufahamu chochote juu ya maisha ya Maimam na nafasi yao katika maisha, isipokuwa dondoo za kihistoria chache, anazozisikia kuhusu ibada za Maimamu au miujiza yao, ambayo inaweza kumfanya azidi kuwa mbali na kuongeza dharau yake, wakati anapopatwa na hisia mbaya.

Hapa ndipo unapokuja wajibu wetu na jukumu letu katika kuwaelimisha vijana wanaoinukia na kuwafahamisha maisha ya Maimam, na mchango wao katika historia na mfumo wao katika maisha, ili watoto wetu wafahamu thamani ya Maimam na wajue wigo wa huduma na kujitolea kwao katika jamii ya kibinadam kwa ujumla, na kwa vizazi vya umma wa Kiislam hususan. Na kitabu hiki ni sehemu ya kwanza katika mlolongo wa vitabu vichache unaotolewa na ofisi ya Rasulil-Adham (saww) al-Amah – Mutwarah, Sultwanatu Umman – kama mchango wake katika kuwaelimisha vijana wanaoinukia na kujaza pengo la kifikira kwa vijana. Na kuelezea juu ya maisha ya viongozi wa umma, na Maimam waongofu (as).

Na sote tunatumai kwamba mlolongo huu uweze kuvutia mtazamo wa vijana wenye kiu ya kuelewa na maarifa, na kupata matarajio yao na matakwa yao. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuwafikishe kufikia malengo yetu na kutekeleza ujumbe wetu, hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

**Hasan Musa as Safar**

بسم الله الرحمن الرحيم

# JUKUMU LA MAIMAMU KATIKA MAISHA

Je, ni sahihi kwamba Maimamu ni kundi tu la wachamungu, ambao hawakuwa na lengo isipokuwa swala, wala shughuli isipokuwa kuvuta tasbihi, wala hawakuwa na kazi isipokuwa dua tu? Na ikiwa hawakuwa na mchango wowote nini sababu ya kuwepo kwao kama Maimamu? Na kwa nini walikuja na wakaishi? Tunaweza kujua jukumu la Maimamu katika maisha na kazi yao katika historia ndani ya maudhui yafuatayo:

## MAIMAM NI UTEKELEZAJI WA MISINGI:

Kuna misingi mitukufu ya kibinadamu, anayoipenda kila mtu, na inayoihitajia kila jamii, na kila mtu anaitumaini, hakika ni misingi ya kheri, wema na ukamilifu kama vile uadilifu, haki, ikhilasi, kujitolea, na kuwahudumia wengine. Misingi hii kwa utukufu wake na kwa ugumu wa kulazimiana nayo, hakika ni nadra kuwepo katika uhalisia wa kiutendaji hadi ionekane kwa mwanadamu: Kana kwamba ni nadharia za mfano au fikra tupu na ni ndoto za mchana, na kwamba uhalisia wake na utekelezaji wake ni kitu kisichowezekana maadamu mwanadamu ni mwanadamu yule yule kwa matamainio yake, raghaba zake na hawaa zake. Na mfano wa dhana hii, mwanadamu anaburudika kwa sababu inatengeneza kisingizio cha kuikosea misingi hii na kutoka katika mipaka yake, kwani yeye haoni nafsi yake wakati huo, kuwa ni mwenye kuwajibika kwa kushikamana nayo,

wala hahesabu nafsi yake kuwa ni mwenye wajibu wa kuiheshimu. Na ni wazi kwamba dhana hii ni hatari sana katika wema wa jamii ya kibinadamu, lakini namna gani tutaondoa hatari hii?

Hatuwezi isipokuwa kama tu tutamthibitishia mwanadamu kosa la dhana hii, na tukamuonyesha uhalisia wa misingi hiyo, na uwezekano wa kuitekeleza kwake, na hii haitotimia isipokuwa kwa kuwepo kundi la watu, wanaobeba jukumu la kushikamana na misingi hii, na kuitekeleza katika uhalisia wa maisha, katika wakati ambao watakuwa humo ni watu kama binadamu wengine, katika kumiliki utashi na raghaba.

Na kuwepo kundi hili ambalo linatekeleza misingi hiyo kivitendo, na linavumilia kila gumu katika njia hii, kunatengeneza msukumo wenye nguvu kwa watu wengine wa kushikamana na misingi na kufuata kundi hilo na kushikamana na majukumu yake na misimamo yake. Na katika upande mwingine: Hakika Mwenyezi Mungu anamtaka mwanadamu na atamhisabu siku ya Kiyama kwa kadiri atakavyoshikamana na kulazimiana na misingi hiyo, ikiwa mwanadamu anaitakidi ubora wa misingi hiyo lakini bila kuwepo uwezekano wa kuitekeleza basi atakuwa na hoja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu hatakuwa na haki ya kumhisabu kwa kutokulazimiana na jambo ambalo nafsi yake haioni kuwa hakuna uwezekano wa kulazimiana nalo.

Hivyo ni lazima Mwenyezi Mungu atawalishe katika maisha haya watu miongoni mwa wanadamu watakaosimamia jukumu la utekelezaji na kufanyia kazi misingi hii. Na kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu ameleta Manabii na Maimam, na hili ndio jukumu la msingi katika maisha. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنْذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

**"Mitume wabashiri, waonyaji ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya Mitume."**[1]

Na kwa ajili hiyo tunamwita Imam ni Hujah na tunawaita Maimam *Hujajullahi* (Hoja za Mwenyezi Mungu) kwa viumbe Wake. Na hadithi ifuatayo inatuwekea wazi ukweli huu: Kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (as) amesema: "Ataletwa mwanamke mzuri siku ya Kiyama ambaye alipata mtihani kutokana na uzuri wake. Atasema Mola Wangu umefanya umbo langu kuwa zuri hadi nikapata niliyoyapata (angalia namna gani anazingatia upotovu kuwa ni jambo la kawaida, kwa sababu hawezi kujizuia nao kwa sababu ya kuwepo vishawishi), basi ataletwa Mariam mbele yake kisha ataambiwa: Wewe ni mzuri zaidi au huyu? Tulimjalia kuwa mzuri lakini hakuhadaika. Na ataletwa mwanaume ambaye alipata mtihani kutokana na uzuri wake atasema: Mola Wangu umenijaalia kuwa mzuri hadi nikapata niliyoyapata, basi ataletwa Yusufu (as) na kuambiwa: Wewe ni mzuri zaidi au huyu? Tulimjaalia kuwa mzuri na hakuhadaika. Na ataletwa mwenye maradhi ambaye alipata mtihani kutokana na maradhi yake, atasema: Ewe Mola Wangu ulinizidishia maradhi hadi nikapata mtihani, basi ataletwa Ayubu na kuambiwa: Je, maradhi yako ni makubwa zaidi au maradhi ya huyu? Tulimpa mtihani lakini hakuhadaika."[2]

Jukumu la Maimam ni kama jukumu la Manabii katika maisha, wao wanatekeleza misingi ya kheri na wema na kuibadilisha kwenda

[1] Suratul- Nisai: 165

[2] Muhammad Baaqir al- Majilisiy katika Biharul-Anuwar, Jz.12 chapa ya pili iliyosahihishwa 1403 Hijiria (Beirut Daru ihiyaai turath al – arabiy) uk. 341

kwenye mwenendo wa kivitendo, pamoja na ugumu wote, ili watu wengine wawaige wao. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ

**"Hakika mlikuwa na kigezo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu."[3]**

Na kwa hakika Maimam walisimamia jukumu hili la kheri kwa uzuri kabisa, wakaonyesha mfano mwema - katika historia – katika kushikamana na misingi, na katika mapambano kwa ajili ya kuitekeleza na kuifasiri kivitendo katika misimamo ya kimaisha, na tunaona baadhi ya mifano:

**1. Thamani ya haki:**

Katika upande wa nadharia, watu wote wanaona dharura ya kushikamana na haki, na wanapinga kwenda kinyume na haki, lakini katika vitendo, je watu wote wako tayari kushikamana na haki wakati inapogongana na maslahi yao na malengo yao? Mara nyingi mwanadamu anajua msimamo wa haki lakini anaghafilika nayo, kwa sababu inapingana na maslahi yake, je kuna maslahi au lengo kubwa zaidi kuliko kiti cha utawala, na kiti cha uongozi, utawala wake ni kuanzia kwenye milima ya Yemen hadi mwisho wa mipaka ya Iran, na kuanzia mto Nile hadi mwisho wa ufukwe wa Bahari ya Mediterenia?

Hakika ni maslahi makubwa, ni utawala wenye ushawishi, mwanadamu kuwa mtawala wa sehemu hii pana iliyostawi, kwa kukhalifu kidogo mfumo wa haki. Hakika sisi tunasoma kuhusu watawala wa historia na tunashuhudia watawala wa leo namna gani wanaengua

[3] Suratul- Ahzab: 21

misingi yote na wanaharibu misingi yote na wanaitupilia mbali ikiwa itazuia njia ya utawala wao au itatishia utawala wao, lakini Imam Ali bin Abi Twalib (as) alipewa ukhalifa kwa fursa kubwa na ukubwa wa vigezo kwa sharti la kukhalifu haki, na alikuwa anaweza baada ya hapo kulitengua sharti hilo, lakini alipinga na kukataa ukhalifa.

Na hiyo ni baada ya kuuliwa Khalifa Umar bin al-Khatwab, ambaye aliweka kamati ya kuchagua Khalifa wa umma baada yake, na kamati hiyo ilikuwa inaundwa na watu sita, mmoja wao ni Imam Ali (as) na walipokutana Abdurahaman bin Auf kiongozi wa kamati hiyo alimwambia: Nakupa kiapo cha utii ewe Ali kwa sharti la kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Sunna ya Mtume Wake na sira ya Masheikh wawili, Imam akasema: "Nitakubali kiapo cha utii kwa sharti la kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Sunna ya Mtume Wake na juhudi za rai yangu." Wakamkatalia, basi akakataa ukhalifa na wakampa kiapo cha utii Uthman bin Affan – na vitabu vya historia vimetaja tukio hili na kwa madhumuni haya, miongoni mwayo ni Tabariy na wengineo.[4]

## 2. Thamani ya uvumilivu na kujitoa muhanga:

Hakika ni thamani kubwa mwanadamu kubakia mvumilivu juu ya msimamo wa haki bila ya kujali yanayomgharimu miongoni mwa thamani, na kupinga kukhalifu misingi yake kwa ushawishi wowote, na kuwa tayari kujitoa muhanga kwa mali yake, watoto wake, watu wake, familia yake na maisha yake katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini ni nani anayeweza kutekeleza msingi huu na kutekeleza jukumu hili ili vizazi vya umma viige kwake? Hakika ni Husain bin Ali (a.s.), watu walimzuia maji, wakauwa wafuasi wake na masahaba wake wote, wakamchinja hata mtoto wake mchanga. Na wao wali-

[4] Abu Jaafar Muhammad bin Jarir Twabariy katika *Tarikh Twabariy*, Juzuu ya 3 chapa ya 1410 Hijiria (Beirut Darul-fikri) uk. 297

kuwa wamedhamiria kumuuwa na kuteka familia yake au aachane na msimamo wa kupinga na wa mapinduzi na anyenyekee kwenye utawala wa Yazid na wakati huo ataishi maisha mazuri na ya raha.

Lakini Husain (a.s.) alikataa hilo, la kuachana na misingi yake, na akadhamiria kupambana na kujitoa muhanga kwa kila anachomiliki kwa kusema: "Hapana Wallahi sitowapa mkono wangu kuwapa kwa udhalili, wala sitokimbia kama wanavyokimbia watumwa, hakika mimi najilinda kwa Mola Wangu na Mola Wenu na kila mwenye kiburi asiyeamini siku ya hisabu."[5]

## 3. Thamani ya ikhilasi:

Ni uzuri ulioje mwanadamu kuwa na ikhilasi kwa wananchi wa nchi yake, mwenye kuwajali na kuwahudumia wanyonge katika umma wake na wenye kuhitajia miongoni mwao bila ya kutafuta umaarufu au jaha au hata shukrani kwa kile anachowahudumia! Na ni ugumu ulioje kulea nafsi katika maadili mazuri ya kibinadamu! Soma maisha ya Imam Zainul-Abidin (as) ili uone namna gani alikuwa anatoka usiku, wakati giza linapotanda na watu kulala fofofo na ukimya kutawala, Imam anatoka na mgongoni mwake amebeba mifuko ya chakula au kiriba cha maji au mzigo wa kuni na kwenda kwenye nyumba za mafakiri na wenye haja, anagonga milango yao taratibu, na anapotoka toka humo yeyote miongoni wa watu nyumba, wenye kuhitajia anampa mahitaji yake ilihali amejifunika ili asijulikane na anaondoka haraka kwenda kwenye nyumba nyingine, na fakiri anajaribu kumtambua huyu mkarimu mwema ili amshukuru na amtaje kwa kheri, anauliza wewe ni nani Mwenyezi Mungu akulipe kheri? Imam anasema: Ni mja kati ya waja wa Mwenyezi Mungu, muombee maghufira na msamaha kwa Mwenyezi Mungu.

Na Imam Zainul-Abdin alikuwa na mtoto wa ami yake ambaye

[5] *Biharul-Anuwar,* Juz. 44, uk. 191

alikuwa akimuudhi Imam, lakini Imam alikuwa anampa dinari usiku ilihali amejifunika, na ndugu yake huyo alikuwa anasema: "Lakini Ali bin Husain haungi udugu wangu, Mwenyezi Mungu asimlipe kheri" Imam anamsikia na anavumilia na wala hamdhihirishii nafsi yake. Na Imam Zainul-Abdin alipofariki na ukakatika msaada wake kwa mafakiri na wenye kuhitajia ndipo watu wakajua kwamba yeye ndiye aliyekuwa anafanya kazi hiyo.[6] Na sasa hivi na kwa kupitia mifano hii iliyotangulia je, tumeshafahamu umuhimu wa jukumu hili la Maimamu watukufu na kazi yao? Hakika wao ni kundi la binadamu katika kutekeleza maadili matukufu na misingi mizuri, hakika wao ni kigezo kwa ajili ya vizazi vya kibinadamu vinavyoendelea, hakika wao ni hoja za Mwenyezi Mungu kwa viumbe.

[6] Muhammad bin Muhammad bin Nuuman al-Mufid katika *Irishadu fiy maarifati hujaji llahi alaal-ibaad*, Juz. 2 (Beirut: Tahaqiq Muasasatu Aal al-bait litahaqiqi turathi) uk. 149.

# MAIMAMU NI VIONGOZI WA KISHARIA

Kitu muhimu unachokihitaji umma ni kuwepo uongozi wenye hekima, na serikali adilifu inayowapatia watu mazingira ya uadilifu, amani na uhuru, na kuwaongoza wananchi katika njia ya maendeleo na mafanikio. Umma unapopata balaa la kuwa na uongozi potovu, na serikali dhalimu hakika maisha yake yatageuka kuwa ni Jahannam kutokana na mateso, hofu, dhulma na hatima yake kwa hakika ni kutoendelea na ni kuporomoka. Na jambo linazidi umuhimu na mazingatio wakati wa maporomoko ya kihistoria na nyakati ngumu ambazo umma unazipitia. Na umma unapopata uongozi wenye uelewa na wenye hekima, uongozi huo unaweza kuuvusha umma katika maporomoko hayo na kuuvusha katika hali hiyo, kwa kheri na salama, vinginevyo mustakabali wa umma unatishiwa na mparaganyiko na maporomoko.

Hakuna shaka kwamba miongoni mwa maporomoko ya kihistoria ambayo umma wa Kiislam uliishi nayo ni kufariki Mtume Muhammad (saww) katika mwanzo wa mwaka wa kumi na moja hijiria, kwa sababu kuondoka Mtume Muhammad mwenye ujumbe na mlezi wa umma, kumeleta pengo kubwa katika maisha ya umma, na kwa kuwa maadui wa dola ya Kiislam yenye kukua walikuwa wanasubiria fursa ya kuimaliza na kumaliza kabisa matumaini ya ujumbe wake, ambayo yanatishia madaraka yao, na kwa upande mwingine hakika umma wa Kiislam ulikuwa haujakamilisha upevu wake na ulikuwa bado haujapata hadhi yake kamili katika malezi ya ujumbe, na hayo ni kwa sababu ya ufinyu wa wakati na mazingira ya vita na ugumu wa kazi ya mageuzi.

Katika maporomoko hatari kama haya, Uislam umeandaa nini miongoni mwa dhamana? Na nini ametoa Mtume miongoni mwa utatuzi, utakaoushika umma mkono kwenda kwenye ufukwe wa amani, maendeleo na usalama? Je, inajuzu Uislam nao ndio msingi wa jumla usahau msimamo huu na kuiachia bahati nasibu? Je, inaingia akilini kwamba Mtukufu Mtume (saww) alighafilika juu ya kutokea hali hii? Au alikuwa hajali mustakabali wa ujumbe?

Hakika mwenye kusoma historia ya Kiislam anagundua haraka kwamba matukio yake yalikuwa yanatokea kwa namna isiyo na maandalizi na ujumbe kutokuwa na jukumu lolote katika kutengeneza matukio na misimamo hiyo.

Kabla Mtukufu Mtume (saww) hajazikwa walikutana Answar, watu wa Madina ili wafikirie mustakabali wa dola ya Kiislamu au mustakabali wao katika dola, na wakakumbuka nafasi yao kubwa katika kuunusuru Uislam na kumhami Mtume, basi wakakimezea mate cheo cha ukhalifa wa Kiislam, lakini wao hawakuwa kabila moja wala kundi moja bali walikuwa makabila mawili baina yao kuna historia ndefu ya ushindani, mzozo na vita na haukumalizwa isipokuwa na Uislamu. Hapa zikachemka chuki za zamani na yakadhihiri mabaki ya ugomvi na ushindani baina ya viongozi wa makabila mawili: Sa'ad bin Ubadah kiongozi wa Khazraji na Asiyad bin Hadhiir kiongozi wa Ausi.

Na yakatokea majadiliano makali baina ya makabila mawili, na hayakukatika isipokuwa kwa kuingia baadhi ya masahaba kutoka katika Muhajirina nao ni Abu Bakri, Umar na Abu Ubaidah bin al-Jarrah, wakati huo ukageuka ugomvi na ikhitilafu kutoka kwa Khazraji na Ausi na kuwa wa Answari na Muhajirina, kwani Masahaba Muhajirina walizungumza juu ya haki yao ya ukhalifa mbele ya Answari na baada ya mjadala mkali Abu Bakri alishinda msimamo huu kwa kumpendekeza Umar bin al-Khattab na Abu Ubaidah bin

al-Jarrah kwa kusema: "Nimesharidhia kwenu mmoja kati ya wanaume hawa wawili, yeyote mtakayemtaka basi mpeni kiapo cha utii." Haraka Umar na Abu Ubaidah wakasema: "Hapana, Wallahi hatutatawalisha jambo juu yako, nyoosha mkono tukupe kiapo cha utii!" Basi wakampa kiapo cha utii. Na ili Ausi wadhoofike, upande wa mshindani wao al-Khazraj ukafanya haraka kumpa kiapo cha utii Abu Bakri na hivi ndivyo yalimalizika maudhui ya ukhalifa wa Kiislam katika wakati huo nyeti.[7]

Na Abu Bakri alipojiwa na mauti alimwita Umar bin al-Khattab na akamteua kuwa Khalifa baada yake, na akautaka umma unyenyekee kwake.[8] Na Umar alipojeruhiwa alikusanya watu kati ya masahaba nao ni: Ali bin Abi Twalib, Uthman bin Affan, Twalha, Zuberi, Sa'ad bin Abi Waqasi na Abdurahman bin Auf, na akawaamuru wakutane baada ya kufariki kwake na waafikiane juu ya ukhalifa wa mmoja wao na rai ya mwisho iwe ni ya Abdurahman bin auf.

Na walikutana na baada ya mazungumzo na majadiliano Abdurahman alimgeukia Imam Ali kwa kusema: "Nakupa kiapo cha utii kwa sharti la kufuata Kitabu cha Mwenyezi, Sunna ya Mtume Wake na sira ya masheikh wawili." Imam akasema: "Bali kwa sharti la kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Sunna ya Mtume Wake na ijitihadi yangu." Abdurahaman hakukubali. Akamgeukia mkwe wake Uthamn na akamwambia kama alivyomwambia Ali: "Nakupa kiapo cha utii kwa sharti la kufuata Kitabu cha Mwenyezi, Sunna ya Mtume Wake na sira ya masheikh wawili." Uthman akasema: "Naam." Basi yeye akawa ndio Khalifa.

Na Khalifa Uthman aliuliwa baada ya mapinduzi makali, na watu wakaja kwa Ali bin Abi Twalib wakitamani akubali ukhalifa, na baada ya kumhimiza na kumshinikiza aliafiki ombili lao, na aka-

---

[7] *Tarikh Twabariy* Juz. 2, uk. 444
[8] Rejea iliyotangulia Juz. 2, uk. 618

chukua ukhalifa. Lakini Bibi Aisha na Muawiya walipinga ukhalifa wake na vilevile Twalha na Zuberi walitengua kiapo chao na kutoka, na hivyo vilitokea vita vitatu vikali, ambamo maelfu ya Waislamu walifariki.

Na Imam Ali (as) alipofariki shahidi watu walimpa kiapo cha utii mtoto wake Imam Hasan (a.s.) isipokuwa Muawiya aliongoza jeshi kubwa, na Imam Hasan akalazimika kufanya suluhu na Muawiya na akamwachia utawala. Muawiya akawa ndio khalifa wa Waislamu na katika mwaka wa mwisho wa maisha yake akalazimisha mwanae Yazid awe Khalifa wa umma baada yake. Na ukhalifa wa Kiislam ukabadilika na kuwa ufalme wa kurithiana, umezingirwa katika kabila la Bani Ummayya. Hadi Bani Abbasi walipofanya mapinduzi dhidi yao wakachukua utawala na ukawa ni miliki yao wanarithiana na wanawapasia watoto wao.

Hivi ndivyo ilivyokuwa historia ya Kiislamu, na hivi ndivyo yalivyotokea matukio yake yenye kutia uchungu. Je, kuna Mwislamu mwenye uelewa anaridhia yote yaliyotokea na anafurahia mwenendo wa historia hii? Na ikiwa yaliyotokea ni jambo linalosikitisha na chungu nini badala ambayo ilikuwa ni wajibu itokee? Na nini ufumbuzi ambao dini iliutoa ili kuzuia kutokea matatizo haya, ambayo yaliondoa nguvu ya umma na yakaondoa haiba yake na kuutumbukiza katika dimbwi la kutoendelea, maporomoko ambayo unaishi nayo hadi sasa?

Ni sahihi kwamba sisi hatuwezi kubadilisha yaliyotokea, yaliyotokea yamekwishapita na wala hatuwezi kurekebisha humo, lakini tunakuta nafsi zetu mbele ya moja kati ya mambo mawili: Ama tuitakidi kwamba hakuna uwezekano bora zaidi kuliko ilivyokuwa, na kwamba Uislam haukuwa na njia mbadala ya kuhami mustakabali wa umma na kwamba Mtume (saww) hakuwa anafikiria yatayotokea baada ya kufariki kwake au hakujua katika akili yake kwamba kili-

chotokea kitatokea,[9] na kwa hiyo tutakuwa tumekiri katika dini yetu kushindwa na kuwa Nabii wetu ni mwenye mtazamo finyu. Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu na hayo!

Na ama tuitakidi kwamba kuna badala iliyoletwa na Uislam na kwamba Mtukufu Mtume (saww) alikwishafikiria mustakabali wa umma wake na ujumbe wake na akaweka dhamana ya kutosha ya kuhami ujumbe, na usalama wa umma, lakini ambayo yalitokea yalikuwa ni matokeo ya aina ya taawili au kutoelewa maagizo ya Mtume, na kisha lilikuwa ni kosa ambalo mazingira yalisaidia kutokea kwake, na kwa hivyo tunaweka mikono yetu katika shina la matatizo ya umma na sehemu ya udhaifu katika historia yake, nalo ni kosa la maarifa au utekelezaji wa mafunzo ya dini katika nyanja ya uongozi na utawala.

Na sasa ni nini badili ambayo Uislamu umeiandaa? Na nini utatuzi ambao ameutoa Mtume, wa tatizo la ukhalifa na utawala? - Tunaitakidi kwamba Mtume Muhammad (saww) amefanya kazi tangu mwanzo wa daawa yake, na kwa mkakati wa mbinguni, alilea na kuandaa mtu wa pili anayefaa kwa uongozi wa umma na kuziba pengo baada ya yeye kuondoka, na mtu huyu ni Ali bin Abi Twalib, mtoto wa ami yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na mume wa binti yake Fatima, Mtume alimlea tangu udogoni mwake na akamlea katika mikono yake na akatengeneza nafsi yake kulingana na malengo yake na akatengeneza tabia yake kulingana na misingi yake, na anatusimulia juu ya mazingatio haya

[9] Kuna Hadithi nyingi kutoka kwa Nabii (saww) zinatoa habari ya yatakayotokea katika umma baada ya kufariki kwake (saww) mfano: "Itakuja fitina kama kipande cha usiku chenye giza, mwisho wake unafuata mwanzo wake" Ahmad bin Hanbal katika *Musnad Ahmad bin Hanbal*, Juz. 3, (Beirut Daru Swaadir) uk. 489.
Na amesema (saww): "Mtafuata nyendo za waliokuwa kabla yenu shibiri kwa shibir na dhiraa kwa dhiraa hadi kama wataingia katika shimo la kenge mtawafuata." Muhammad bin Ismail al-Bukhariy katika *Sahihul-Bukhariy* kitabul- Ambiyai babu maa dhukira an bani Israil (Beirut Darul-fikiri).

maalum Imam mwenyewe anasema: “Na mmeshajua nafasi yangu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa ukaribu wa ukuruba na nafasi mahususi, aliniweka katika mapaja yake na mimi nikiwa mtoto, ananikumbatia katika kifua chake na ananilaza katika kitanda chake na ananigusisha mwili wake na ananinusisha jasho lake, na alikuwa anatafuna kitu kisha ananilisha na hajakuta kwangu uongo katika kauli wala kasoro katika kitendo, na Mwenyezi Mungu alishamwekea tangu utotoni mwake malaika mtukufu kati ya malaika watukufu anayemuongoza njia ya mema na tabia njema usiku na mchana, na nilikuwa namfuata kama mtoto anavyomfuata mama yake na ananinyanyua kila siku daraja ya elimu katika tabia yake na ananiamuru kuifuata, na alikuwa kila mwaka anakwenda katika pango la Hiraa namuona na ananiona na wala hamuoni yeyote, na ilikuwa haijakusanya nyumba yeyote siku hizo Waislamu isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Khadija na mimi nikiwa watatu wao, naona nuru ya wahyi na ujumbe na nanusa harufu ya utume.”

Na nilisikia kilio cha shetani uliposhuka wahyi kwake (saww) nikasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nini sauti hii? Akasema: ‘Huyu ni shetani amekwishakata tamaa ya kuabudiwa, hakika wewe unasikia ninayosikia na unaona ninayoyaona isipokuwa wewe sio Nabii lakini ni msaidizi na hakika wewe uko katika kheri.’”[10]

Na amepokea An-Nasai kwamba amesema: “Nilikuwa na nafasi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwa nayo yeyote kati ya viumbe, nilikuwa namwendea kila usiku na nasema: Asalam Alaika Yaa Nabiyallah, akiunguruma narejea kwa ahali yangu, vinginevyo

[10] *Nahjul-Balaghah,* Juz. 2, uk. 157 ya Ibnu al-Hadid; katika sharhu ya *Nahajul-balagha* iliyohakikiwa na Abu al- Fadhil Ibrahim Juz. 13 chapa ya kwanza 1378 Hijria (Beirut Daru ihiyaai al-kutubi al-arabiya Isa al-Baaliy al- hiliy na ameshirikiana naye katika tahakiki Muhammad Abu al-Fadhal Ibrahim) uk. 197.

naingia kwake."[11] Na imepokewa pia kutoka kwa Imam kauli yake: "Nilikuwa na nyakati mbili za kuingia kwa Nabii, wakati wa usiku na wakati wa mchana."[12] Na mara nyingine anasema Imam Ali (as):

"Amenifundisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) Milango elfu moja, kila mlango unafunguliwa milango elfu moja mingine."[13]

Na kwa maandalizi haya ya kiujumbe na malezi ya kiungu Imam Ali amekuwa ni mwenye kustahiki uongozi wa umma kwa ajili ya kuendeleza malezi yake, malezi ya Kiislam yenye kuongoza, Mtume wa Mwenyezi Mungu alitoa tamko kwake la kumteua kwa ajili ya ukhalifa katika zaidi ya sehemu moja, kwa kuanzia na kisa cha indhari (kuonya) pale alipomwambia "Wewe ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu baada yangu."[14] Na kumalizia na tukio mashuhuri la Ghadir khum alipohutubia Mtume wa Mwenyezi Mungu Waislam ambao walihiji pamoja naye Hija ya kuaga kwa kusema: "Je, mimi si mbora kwenu kuliko nafsi zenu?" Wakasema: "Ndio." Akasema akiwa ameshikilia mkono wa Ali: "Ambaye mimi ni kiongozi wake, basi huyu Ali ni kiongozi wake. Ewe Mwenyezi Mungu mpende atakayemtawalisha na mfanye adui atakayemfanyia uadui, mnusuru mwenye kumnusuru na mfedheheshe mwenye kumfedhesha na izungushe haki pamoja naye popote atakapozunguka."[15]

Na vilevile Imam Ali alizingatia malezi ya watoto wake Hasan na Husain ili awaandae kwa ajili ya uongozi wa umma baada yake.

---

[11] Abu Abdurahman Ahmad bin Shu'aib Anasaai katika *Sunan al-Kubra* Juz. 1 chapa kwanza 1411Hijiria (Beirut Darul-kutubil- ilimiyah) uk. 360

[12] Rejea iliyotangulia uk. 141

[13] Alau Diyn Ali al-Mutaqiy bin Hasaam Diyn al-Mutaqiy al-Hindiy katika *Kanzul-Umaal* Hadith namba 36372 (Beirut Muasasatu Risalah, kimehakikiwa na Sheikh Bikiriy Hayaaniy, sheikh Swafuwatu Saqaa) uk. 114

[14] *Tarikh Twabariy* Juz. 2, uk. 63

[15] Imepokewa kwa matamshi mbalimbali rejea, kwa mfano: Ahmad bin Hanbal katika *Musnad Ahmad bin Hanbal* Juz. 4, uk. 281, Muhammad Naswir Diyn al-Albaaniy katika *Silsilatu Ahaadith sahiha*, hadith namba 2982

Na Husain alifanya kazi ya kumlea mtoto wake Zainul-Abidin, Na Zainul-Abidin alizingatia kumwandaa mtoto wake al-Imamul-Baaqir, na vivyo hivyo hadi kwa Imam al-Hujah Imam wa kumi na mbili. Na hii haimaanishi kwamba sisi tunaamini njia ya utawala wa kurithiana, kwani kurithiana sio stahiki ya kweli ya uimamu, vinginevyo kwa nini uimamu ulihamia kwa Imam Musa al-Kaadhim na haukuwa kwa ndugu yake mkubwa Abdillahi au Ismail?

Bali uimam ni uteuzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu pamoja na kumwaandaa Imam na kumlea kwake kwa malezi elekezi. Na alikwishataka Mwenyezi Mungu uongozi wa umma utokane na nyumba zake takatifu nayo ni nyumba ya Mtume Muhammad (saww), na ametaka Imam azaliwe na Imam aliyetangulia, atakayesimamia malezi yake na maandalizi yake kwa njia bora.

Na hapa lazima tutilie mkazo kwamba jukumu la kawaida la Maimamu ni uongozi wa umma, uongozi wa hekima na mzuri, unaofungua njia ya wema na maendeleo kwa umma, na kuondoa kwao matatizo na shida, lakini kwa masikitiko makubwa hawa Maimamu hawakupewa fursa ili watekeleze jukumu lao, na kutekeleza ujumbe wao katika maisha ya umma. Na kama mazingira yangewaruhusu na umma ukanyenyekea na wakaweza kufika katika kiti cha hukumu na utawala umma ungekuwa na historia isiyokuwa historia hii, na hali yao isingekuwa hali hii.

# MAIMAMU NA JUKUMU LA UJUMBE

Ujumbe wa Kiislam ni wenye kudumu, ambao Mwenyezi Mungu ameuandaa kama mfumo kamili kwa binadamu hadi mwisho wa maisha. Ujumbe huu kamilifu ambao unapamba maisha ya binadamu na unapangilia harakati zake zote, na unapangilia misimamo yake ya kifikira, kisiasa, kiuchumi na kijamii, je hauhitajii marejeo yenye kubeba jukumu na kuusambaza, na kubainisha hukumu zake na kufafanua rai zake na kuondoa kwake uadui kutoka nje na kuuhami kutokana na upotovu na uongo? Nabii (saww) alikuwa anasimamia jukumu hili katika maisha yake, kwani yeye ndiye mwenye jukumu la kueneza ujumbe, na ni Marejeo kwa ajili ya ufafanuzi wa makusudio yake na mafunzo yake, na mwenye kukusudiwa katika kuulinda kwake na kuutetea kwake.

Lakini baada ya Nabii (saww) nani ataziba pengo hili na nani atafanya kazi ya kubeba jukumu hili? Uislamu ulikuwa unapambana na jamii mbalimbali kwa misingi yake, ada zake na mila zake, na hili ni jambo linaloweza kupenyeza fikira na ada za jamii hizo katika jamii ya Kiislamu. Na maadui wa Uislamu hawatozembea dhidi ya kuchochea shubuhati na shaka katika daawa mpya. Na jamii ya Kiislam kwa ndani haiepukani na jaribio la ushawishi na upotoshaji ambao kila ujumbe uliotangulia ulikutana nao. Na juu ya hayo yote Waislamu watakutana na mengi kati ya matukio na mambo mapya, ambayo Qur'ani haijayazungumzia na wala Mtume (saww) hajayazungumzia kwa namna ya wazi, namna gani wataamiliana nayo na vipi watajua rai ya Uislamu humo?

Inaweza kujitokeza katika akili kwamba sahaba na maulamaa wa umma wanaweza kubeba jukumu hili baada ya kuwa wameishi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na wamesikia ha-

dithi zake na wamejua misingi yake. Lakini kama tutachukulia katika hesabu yetu masafa ya muda mfupi, ambayo waliishi masahaba pamoja na Mtume (saww) na ambayo hayakuzidi muda wa muongo mmoja (miaka kumi), kipindi ambacho ndio muda ambao unaunda jamii ya Kiislam huko Madina, na humo zilishuka sharia nyingi na kanuni za Kiislam, na tukaona upeo wa matatizo na matukio ambayo yalikuwa yanaikumba jamii hiyo yenye kuinukia, na matatizo hayo kuchukua mazingatio yake na wakati wake mwingi, tutagundua kwamba wakati na mazingira hayakuruhusu sahaba kuelewa ujumbe kwa uelewa kamilifu, na haukumuwezesha kujua mafunzo yote na hukumu zote. Hii ni kwa kufumbia macho yale ambayo yatatokea katika mustakabali wa umma miongoni mwa mambo mapya.

Na unaweza kuhisi ukweli huu kwa kuangalia kwa haraka ikhitilafu za Masahaba katika kutekeleza hukumu za kisharia, hata za kiibada baada ya kufariki Mtume (saww), mfano: "Amepokea Twahawiy kutoka kwa Ibrahim amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu alipofariki watu walihitalifiana katika takbira za jeneza, huachi kusikia mtu anasema nimesikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anatoa takbira saba, na mwingine nimesikia Mtume wa Mwenyezi Mungu anatoa takbira tano, na mwingine anasema nimesikia Mtume anatoa takbira nne, wakahitalifiana katika hilo hadi akafariki Abu Bakri."[16]

Na sira ya Masahaba na vitendo vyao mukabala wa yaliyotokea miongoni mwa matatizo, ni dalili juu ya kuthibiti ukweli huu kwani ilikuwa "Sunna ya Makhalifa wawili Abu Bakri na Umar ni kwamba linapotokea jambo na hawajui chochote kuhusu hukumu yake katika sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), wanawakusanya wajuzi na kuwauliza na kama wakipata kwao sunna wanaichukua,

[16] Ahmad bin Muhammad bin Salamah kutoka kwa Abdul-Maliki bin Salamah al-Twahawiy katika *Sharhu Maaniy al-Athari* Juz. 1, chapa ya kwanza 1399 Hijiria (Beirut: Darul-kutubi al-ilimiyah) uk. 495

na kama ikikosekana wanafanya ijitihadi, na kama wakifanya ijitihadi na wakaafikiana basi hiyo inakuwa ni kongamano na ni wajibu kwa wote kuchukua, na kama wakijitahidi na wala hawakuafikiana, Gavana akiamuru kufuata rai fulani, inakuwa ni wajibu kumtii, hata kama halijapatikana kongamano wala amri, kila mmoja anafanya inavyomuongoza ijitihadi yake. Na sunna ya Makhalifa wawili katika hili ilikuwa ndio sunna ambayo anaifuata kiongozi wa kila mji, ikiwa jambo halitapelekwa kwa Khalifa."[17]

Na unaweza kudhani kwamba alichokifanya Sahaba cha kurejea kwenye ijitihadi ni utatuzi salama na sahihi, lakini namna gani tunaweza kuwa na uhakika au na matumaini kwamba rai ya Sahaba huyu au ijitihadi hiyo imeafikiana na aliyotaka Mwenyezi Mungu na imepatia jambo la kisharia mia kwa mia? Ambapo uwezekano wa kukosea ni jambo la kawaida katika ijitihadi, ingawa kosa linasameheka kwa mujitahidi mbele ya Mwenyezi Mungu, lakini bado haijatufikisha kwenye hukumu halisi ambayo ametuamuru Mwenyezi Mungu.

Pili: Wakati dini isipoainisha Marjaa mmoja, na Imam mwenye kutiiwa na ambaye umma utarejea kwake na kupata matumaini kwenye rai yake, je hiyo haimaanishi kuwa ni kuwa na rai nyingi na ikhitilafu za ijitihadi? Ni rai ya nani umma utaitegemea? Na wakati huo nani atahakikisha kwamba ikhitilafu hii ya rai haitageuka na kuwa ugomvi unaovunja umoja wa umma, kufarikisha safu zao kama ilivyotokea? Ambapo kumekuwa na madhehebu mengi na rai zimegongana hadi baadhi yake wamekuwa wanakufurisha wengine, na wanawahukumu kwa ufasiki na kutoka katika dini?

Imekwishabainika wazi kwetu kwamba utatuzi salama na tiba inayofaa ambayo inatuhakikishia rai halisi ya kidini na inayotupatia umoja na kongamano ni kuwepo Imam anayebeba jukumu hili

[17] *Masu'atu Jamaali Abdu Naaswir fiy fiqihil-Islaamiy* Juz. 1, uk. 25

kwa uwezo na ushujaa, na umma unanyenyekea kwake, na anafanya jukumu lake la kuuelewesha na kuuelimisha umma, na kubainisha rai ya dini katika mambo mapya yanayojitokeza miongoni mwa matatizo na kuuhifadhi ujumbe kutokana na maadui na wapotoshaji. Na hili ndio hasa jukumu la Maimam watoharifu ambao tunaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaandaa kwa ajili ya kufanya kazi hii, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawateua ili kubeba jukumu lake na alikwishasema Mtukufu Mtume (saww) kwa maafikiano ya Waislamu na maulamaa wao: "Hakika mimi nimewaachia vizito viwili kimoja wapo ni kikubwa kuliko kingine, Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kamba iliyonyooka toka mbinguni hadi ardhini, na kizazi changu, Ahlulbayt wangu, hakika hivyo havitotengana hadi vitakaponijia katika hodhi yangu."[18]

Na katika riwaya nyingine: "Hakika mimi nimewaachia ambayo kama mtashikamana nayo hamtapotea kamwe baada yangu, kimoja wapo ni kitukufu kuliko kingine: Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kamba iliyonyooka toka mbinguni hadi ardhini  na kizazi changu Ahlulbait wangu, havitotengana hadi vitakaponijia kwenye hodhi, angalieni namna gani mtanifuata katika hivyo."[19]

Na ambapo mazingira hayakuruhusu Maimam wa Ahlul-bayt kufanya jukumu lao la kawaida katika kuongoza umma na kuuelekeza, kueneza ujumbe na kuuhami, isipokuwa walikuwa (as) wanapopata fursa wanaitumia katika nyanja mbalimbali ili kufanya kazi yao na jukumu lao katika kufafanua mafunzo ya Uislamu na kuweka wazi misingi yake, na nitanukuu dondoo na mifano kwa muhtasari inayoelezea juu ya Maimam kubeba jukumu hili na kufanya kazi hii:

[18] *Musnad Ahmad bin Hanbal,* Juz. 3, uk. 14

[19] Muhamad bin Isa bin Surah *Tirmidhiy,* Juz. 5, uk. 329, chapa ya 1403Hijiria (Beirut Darul fikir kimehakikiwa na Abdul-Wahab Abdu Latif), *Silsilatu al-Ahaadith sahih* Juz. 4, uk. 355 – 358.

# KADHIA YA KISHARIA

Binti mwenye kujihifadhi alimaliza muda wa ukapera katika maisha yake, kwa uaminifu na kujihifadhi, ambapo aliolewa na mmoja wa Waislamu, kudra ikataka ajifungue baada ya kupita miezi sita na masiku kadhaa kwa mume wake. Ni jambo la kawaida kwa watu kwamba muda wa mimba haupungui miezi tisa, hivyo binti huyu mtukufu akatuhumiwa na akawa ni gumzo katika ndimi za watu ambao wanafuatilia makosa ya wengine na aibu zao, ambapo mume wake alilazimika kupeleka jambo hili kwa Khalifa Umar bin al-Khattab, lakini Khalifa naye pia alikuwa anaitakidi kama watu wengine: kwamba muda mchache wa mimba ni miezi tisa! Hakuchelewa kumhukumu kwa adhabu ya zinaa!

Wakamshtukiza kwa hukumu ya Khalifa dhidi yake, hukumu ya adhabu, moyo wake ukapasuka kwa uchungu, kwani alikuwa ana uhakika juu ya utukufu wa nafisi yake na kuhifadhi heshima yake. Na hapa akaishi katika mkanganyiko wa kinafsi na mvutano mkali wa ndani, vipi Mwenyezi Mungu amenikadiria mimi kuzaa baada ya miezi sita kisha ananihukumu kwa adhabu? Mimi nini dhambi yangu? Vipi kudura yake ya kimaumbile inaweza kupingana na hukumu ya kisharia ya Mwenyezi Mungu? Je, ni sahihi kwamba hii ni hukumu ya Mwenyezi Mungu au hukumu ya khalifa imekosea? Hivyo nani atanihami heshima ya watu na utukufu wao na mfano wa makosa haya?

Mwenyezi Mungu alitaka binti huyo asiye na hatia aokolewe na kuthibitisha kwake uadilifu wa sharia Yake na kushikamana kwake na kanuni za kawaida, na Mwenyezi Mungu alitaka kuweka wazi ukweli huu na kudhihirisha haki. Imam Ali bin Abi Twalib alipita na kuona watu wamekusanyika, wanangojea kutekelezwa adhabu kwa

yule binti mwenye kujihifadhi. Akauliza juu ya habari, wakamjulisha kwamba binti hajamaliza miezi sita tangu kuolewa kwake na sasa hivi ameshajifungua. Imam akawakata kauli yao: Na kuna nini katika hilo? Wakasema: Hakika inaonyesha kwamba yeye amezini kabla ya kuolewa kwa muda wa miezi mitatu, na hivyo Khalifa amekwishahukumu adhabu ya kupigwa mawe (*hadd*). Imam akahisi uchungu sana na akamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika kwake kabla ya kutekelezwa hukumu kwa binti aliyedhulumiwa na akasema: Subirini hadi nirudi kwenu.

Akaenda haraka kwa Khalifa Umar na akamuuliza juu ya tegemeo lake katika kumhukumu kwake kwa adhabu hiyo. Umar akasema: Kwa sababu mimba haiwi ya mieizi sita. Imam akajibu: Hakika Qur'ani inakiri kwamba muda mchache wa mimba ni miezi sita. Umar akasema: Iko wapi katika Qur'ani? Imam akafafanua: Hakika ni kauli yake (swt):

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا
وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا وَحَمْلُهُ وَفِصَالُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا

**"Na tumemuusia mtu awafanyie wema wazazi wake wawili. Mama yake amebeba mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba kwake na kumwachisha ziwa ni miezi thalathini."** [20]

Hivyo imekiri kwamba muda wa mimba na kunyonyesha ni miezi thelathini. Miaka miwili na miezi sita. Na katika aya nyingine Mwenyezi Mungu anabainisha muda wa kunyonyesha au kuachishwa ziwa ni miaka miwili kamili:

[20] Suratul- Ahqaaf: 15

وَفِصَالُهُ فِي عَامَيْنِ

**"Na kumwachisha kwake ziwa ni baada ya miaka miwili."**[21]

وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ

**"Na wazazi wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili."**[22]

Ikiwa tutaondoa muda wa kunyonyesha na kuachishwa ziwa katika jumla ya muda wa mimba na kuachishwa ziwa (30 – 24 = 6) basi miezi sita iliyobakia ndio muda wa mimba kwa mujibu wa Qur'ani. Khalifa akaafiki rai ya Imam na hapo akasema kauli yake mashuhuri: 'Kama si Ali, Umar angeangamia,' na binti akaachiwa.[23] Je umeona namna gani Imam alivyotatua tatizo hili la kijamii ambalo linaweza likajirudia? Na namna gani aliweza kubainisha rai ya dini katika kadhia hii? Katika mfano wa misimamo hii linadhihiri jukumu la Maimam, na hapa unaonekana upande huu katika thamani yao halisi (as).

## HAKUNA KUNYAMAZIA DHULMA:

Katika wakati wa mwanzo umma wa Kiislamu ulipata balaa ya utawala muovu, uliopenya hadi katika nafasi ya ukhalifa na utawala, kwa mabavu na ugaidi, kama vile utawala wa Bani Ummayya na Bani Abbas na haukushikamana na dini ya Mwenyezi Mungu wala haukuhukumu  kwa sharia yake katika maisha, ukapora haki za mwananchi na ukampokonya heshima yake na uhuru wake. Na chini

[21] Suratu Luquman: 14

[22] Suratul- Baqara: 233

[23] *Biharul-Anuwar* Juz. 30 uk. 11, Sulaiman Ibrahim al-Hanafiy al-Qanduziy katika *Yanabiul-Mawadatu lidhaway al-Qurbaa* Juz. 2 chapa ya 1416 Hijiria (Darul usuwah kimeahikikiwa na Sayid Ali Jamaal Ashraf Husainiy al- Baihaqiy) uk. 173, Ahmad bin al-Husain al-Baihaqiy, *Sunanul-Kubraa,* Juz. 7, uk. 332 babu Maa jaa fiy aqalil- hamli.

ya kibano cha ugaidi na mabavu na kwa msukumo wa woga na udhalili ikasambaa katika safu za umma hali ya kunyamaza, unyonge, na kujisalimisha, katika hali ya ufisadi.

Na kwamba: Hakika waanzilishi wa msimamo huu wa kushindwa walipaka na kuuvisha msimamo wao huo wa kimabavu na kigaidi vazi la kidini na wakatengeneza kisingizio cha kisharia na wakatoa mafuhumu na fatwa zinazoamuru kunyenyekea na kuishi kwa woga, zinazolingania kunyamaza na kujisalimisha, zinazokataza kupinga na kufanya mapinduzi, na wakazipa nguvu kwa baadhi ya hadithi na nukuu, nazo ama sio sahihi katika sanadi au zilikuwa zinafasiriwa vibaya na kupanga sehemu za utekelezaji wake. Na haifichikani hatari ya mtazamo huu katika Uislamu, na katika maslahi ya umma na mustakabali wake, kwani ni kuimarisha hali ya ufisadi, na kuhifadhi na kuendeleza dhulma na upotovu.

Na hapa Maimam wa Ahlul-Bayt walisimama kwa jukumu lao la kiujumbe na wakapambana kwa ajili ya kupiga vita mtazamo huu wa kujisalimisha na uongo wake, na wakaweka wazi rai ya Uislam ya kimapinduzi, ambayo inapinga dhulma, na inakataa kuinyamazia, na kuinyamazia ni kushiriki kivitendo katika kosa. Na alikwishasimama katika msimamo huu wa Kiislam Imam al- Husain bin Ali (as) ambaye alitangaza mapinduzi dhidi ya dhulma na uovu, na kubainisha rai halisi ya dini dhidi ya ufisadi kwa kusema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amesema: "Mwenye kuona mtawala muovu anayehalalisha haramu ya Mwenyezi Mungu, mwenye kutengua ahadi ya Mwenyezi Mungu, mwenye kukhalifu sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anafanya madhambi na uadui kwa waja wa Mwenyezi Mungu na wala asibadilishe kwa kitendo wala kwa kauli basi ni haki ya Mwenyezi Mungu kumwingiza katika moto."[24]

[24] *Tarikhu Twabariy,* Juz. 4, uk. 304

Na hili ndilo jukumu la mwisho la Maimam katika maisha, nalo ndio lenye hatari nyingi zaidi na lenye umuhimu zaidi, nalo ni jukumu la kubadilisha hali ya kisiasa na kijamii ambayo inatishia mustakabali wa ujumbe kwa hatari ya mparaganyiko na upotovu, na Maimam walikwishabeba jukumu la kubadilisha la kimapinduzi, kwa kila wanayomiliki hadi kwa damu zao na roho zao.

## MISINGI NDIO KIPIMO:

Uislamu ulikwishafanya kazi ya kulea umma wa Kiislamu malezi ya mwanzo yenye uelewa, na ilikuwa kati ya vipimo muhimu ambavyo Uislamu ulivizingatia katika kuyazatiti katika dhamira ya umma ni: Misingi iwe ndio mizani na kipimo cha harakati yoyote au kitendo au tathmini, na watu hawana thamani isipokuwa kwa kiwango cha kushikamana kwao na misingi hiyo, na mtu yeyote anayepotoka au kukhalifu chochote kati ya misingi ya Kiislamu anahukumiwa kwa kosa, yeyote yule awaye na vyovyote kitakavyokuwa kiwango chake. Na umma ukaenda kulingana na vipimo hivi, na kwa kutekeleza msingi huu mtukufu, hata kwa makhalifa na watawala: Khalifa Umar alipotaka kulazimisha kwa watu hukumu ya kimakosa mwanamke wa Kiislamu wa kawaida hakuogopa kusimama dhidi yake kwa kumpinga kwa kutoa hoja ya Qur'ani, jambo ambalo lilimpelekea Khalifa kukiri kosa na kuacha rai yake. Amepokea Abdu Razaq amesema: Umar alisema: Msizidishe sana mahari kwa wanawake. Mwanamke akasema: Hayo sio yako ewe Umar. Hakika Mwenyezi Mungu anasema: "Na mkawa mumempa mmoja wao rundo la mali." Umar akasema: Mwanamke amepambana na Umar na akamshinda.[25]

Na Abu Dharr al-Ghifaariy pamoja na ufakiri wake na unyenyekevu wake, alipoona upotovu na kuchezewa uchumi wa umma,

[25] Shihabu Diyn Ahmad bin Ali bin Hajar katika *Fathu al-baariy*, sharhu ya *Sahihil-Bukhariy,* Juz. 9, chapa ya nne (Beirut Darul-Ihiyaa turathi al-arabiy) uk. 167, *Biharul-Anuwar* Juz. 44, uk. 322, *Kanzul-Umaal,* Juz. 16, uk. 538

katika zama za Khalifa Uthman, haikumruhusu dhamira yake kumchekea na kunyamaza bali alikasirika na kutangaza kupinga kwake kwa yanayotokea na kutaka kurekebisha hali.[26] Na kuwepo kwa mioyo hii katika umma ndio dhamana ya usalama wa misingi yake na umadhubuti wa mwendo wake. Lakini baada ya muda mfupi wa kupanuka dola ya Kiislamu, baadhi ya pande zenye ushawishi zilijaribu kufuta dauru ya msingi huu mtukufu wa Kiislamu ili kuwapa watu binafsi thamani na kuwapa nafasi ya kuchezea na kufanya kwa maslahi yao binafsi, bila ya kufungwa na misingi na maadili, watu wakati huo wakawa juu ya misingi, na vitendo vyao na nyendo zao zikawa ndio vipimo.

Na katika jaribio hili ni kuongeza sifa ya utukufu na ukuu kwa Masahaba wote ambao waliishi pamoja na Mtume (saww) na kutoa visingizio kwa vitendo vya wote, na kuiona misimamo yao na rai zao ndio sahihi vyovyote zitakavyokuwa zimekosea katika misingi, na wakatunga hadithi za uongo na wakazinasibisha kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kama vile kauli yao: “Hakika masahaba wangu ni kama Nyota, yeyote mtakayechukua kauli yake mtaongoka.” Amesema Muhammad Naaswir Diyn al-Albaaniy kuhusu hadithi hii: Hakika ni uongo, na imenukuliwa kutoka kwa Ibnu Hazim katika juzuu ya 6 uk. 83: “Imekwishadhihiri kwamba riwaya hii haithibiti kabisa, bali hakuna shaka kwamba ni uongo kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema katika sifa ya Nabii Wake (saww): “Na hasemi kwa matamanio. Hakika ni wahyi unaofunuliwa.” Ikiwa maneno yake (saww) katika sharia ni haki na yote ni wajibu basi bila shaka ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na ambayo yanatoka kwa Mwenyezi Mungu basi hayakhitalifiani humo, kwa kauli yake (swt): Na kama yangekuwa yanatoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi wangekuta humo ikhitilafu kubwa.”

---

[26] *Tarikhu Twabariy,* Juz. 3, uk. 353 na baada yake.

Na Mwenyezi Mungu amekwishakataza kufarakana na ikhitilafu kwa kauli yake: "Na wala msizozane" hivyo ni muhali Mtume Wake (saww) kuamuru kumfuata kila msemaji katika masahaba (r.a) na miongoni mwao kuna anayehalalisha kitu na mwingine anakiharamisha. Kama ingekuwa hivyo, basi kuuza pombe ingekuwa halali, kwa kumfuata Sumratu bin Jundub, na ingekuwa kula barafu kwa mfungaji ni halali kwa kumfuata Abi Twalaha, na ni haramu kumfuata mwingine. Na ingekuwa kuacha kuoga kutokana na uzembe ni wajibu kwa kumfuata Ali, Uthmani, Twalha, Abi Ayub na Ubayy bin Kaab, na ni haramu kwa kumfuata Aisha na Ibnu Umar na yote haya yamepokewa kwetu kwa sanadi sahihi.

Kisha akarefusha katika kubainisha baadhi ya rai ambazo zimetokea kutoka kwa Masahaba na humo wakakosea sunna, na hiyo ni katika uhai wa Mtume (saww) na baada ya kufariki kwake, kisha akasema katika juzuu 6 uk. 64: "Namna gani inajuzu kuwafuata watu waliokosea na kupatia?"[27] Na ikiwa itasihi hadithi hii hakika wanaondolewa Masahaba wenye kushikamana na misingi ya Nabii, ambapo thamani yao inakuja kwa mshikamano wao huu. Ama ambao waliteleza katika maporomoko ya upotovu na wakaangukia katika madimbwi ya maslahi, haiwezekani ikatekelezwa kwao hadithi hii ili wawe ni kigezo kwa vizazi vya waumini kwa kuishi kwao tu kwa muda pamoja Mtume (saww).

Na Maimam (as) wamesimamia jukumu hili la kufichua kosa hili la upande huu na kukhalifu kwake misingi ya Kiislamu. Huyu hapa Imam Ali (as) anasema: "Hakika haki haijulikani kwa (kuwaangalia) watu, ijue haki utawajua wenye haki."[28] Na baadhi ya

[27] Muhammad Naaswir Dyn al-Albaaniy katika *Silsilatu Ahaadith dha'ifaah*, Juz. 1, uk. 61 chapa ya kwanza 1993 (Riyadh: Maktabatu al-Maarif) uk. 149 -151.

[28] Abu Jaafar Muhammad bin al-Hasan Tuusiy katika *Tibuyaan fiy tafsiril-Qur'an,* Juz. 1 chapa ya kwanza 1409 Hijiria (Maktabul-Ilaamil-Islamiy, kimehakikiwa na Ahmad Habib Qaswir al- Amiliy) uk. 190.

Masahaba walipokuwa ni kikwazo katika njia ya urekebishaji wa Imam Ali (a.s.) baada ya kuchukua kwake Ukhalifa hakuona kizuizi cha kupambana nao na kuwafyeka, ambapo waling'ang'ania katika uasi wao na kutoka kwao katika utawala wake wa kisharia, pamoja na kwamba wao mwanzo walikuwa ni kati ya Masahaba bora wa Mtume (saww). Hivi ndivyo tulivyojua umuhimu mkubwa wa Maimam katika maisha na dauru yao kubwa katika umma kupitia nukta zilizotangulia ambazo ni:

- Kutekeleza misingi
- Uongozi wa kisharia
- Kubeba jukumu la ujumbe.

## SIFA ZA MAIMAMU

Uimam ni cheo kikubwa na jukumu kubwa ambalo juu yake yanasimama maisha ya Maimam na hatima ya ujumbe, je anaweza kubeba jukumu lake mtu yeyote wa kawaida? Au una sifa, vipaji na uwezo ambao ni lazima utimie kwa mtu anayeteuliwa kwa ajili ya Uimam ili aweze kubeba jukumu na uongozi wa umma katika ufukwe wa haki na wema?

Hakika ni lazima Imam awe na uwezo na kipaji cha hali ya juu na lazima awe na sifa maalum, zinazomfanya aweze kushika cheo hiki na kubeba jukumu hilo. Na tutaeleza sasa hivi sifa hizi kupitia mtazamo wa Uislamu na uhalisia wa maisha ya Maimam watukufu ambao historia imeiandika katika kurasa zake zenye nuru.

## UMAASUMU NI DHARURA YA UONGOZI:

Na Umaasumu unamaanisha: Kulazimiana kikamilifu na dini, na kupatia haki daima. - Na hivyo, Umaasumu ni dharura ya uongozi, kwa sababu ni mwenye jukumu la kubainisha mafunzo ya dini, na kueneza hukumu za kisharia na kuzihifadhi na kuzitekeleza. Ni lazima yeye awe ni wa kwanza kulazimiana nazo, vinginevyo vipi watu wataamini uongozi wa ambaye wanagundua upotovu wake katika yale ambayo anawalingania wao kuyatekeleza?

Pili: Kinachotakiwa kwa Imam ni kuwa kigezo kwa wengine, na kauli zake, vitendo vyake, misimamo yake ni hoja kwa watu. Wanafahamu kupitia kwake rai ya Uislamu na misimamo yake, na wakati huo hakika kosa la Imam na kupotoka kwake kutauongoza umma wote kwenye maporomoko ya kukosea na upotovu.

Tatu: Maasi yakijuzu kwa mtu yeyote kati ya watu wa umma, hiyo ni kwa sababu upotovu wake utakuwa katika wigo mfinyu sana na chini ya udhibiti wa kanuni. Ama ikiwa kiongozi wa umma na Imam wa dini anaweza kupotoka, hakika upotovu wake utakuwa ni fedheha na hatari kwa umma wote, na kwa ujumbe wote. Mfano: Ikiwa itasihi kwa Imam kuasi, sasa nani atadhamini asipunje haki za umma? Nani atadhamini asitawaliwe na tamaa na ubinafsi, na hivyo kuhukumu kwa utashi wa maslahi yake binafsi?

Na mwisho: Nani atadhamini kutekeleza kwake hukumu za dini kwa ukamilifu na umadhubuti. Na ikiwa rai zao daima hazipatii, namna gani umma utafuata amri yake, maadamu humo kuna uwezekano wa kukosea? Na wakati huo anakuwa ni Imam wa kundi maalum au mas'ala maalum na sio kwa umma wote na dini yote?

Na kwa kuzingatia Imam ni kiongozi wa umma, hakika maamuzi yake na vitendo vyake ikiwa havitapatia haki hakika vitakuwa ni

balaa kwa umma, ikiwa Imam ni kama mwanachuoni yeyote mwingine anajitahidi na kukosea, hakika thamani ya kosa lake itakuwa kubwa na yenye kuumiza, mfano walipofanya ijitihadi Twalha na Zuberi (kama baadhi wanavyodai) wakakosea, je matokeo yake yalikuwaje? Hakika walifariki watu elfu 40 au elfu 25 na watu elfu 14 walikatwa mikono kama zilivyoeleza riwaya za kihistoria. Na alipojitahidi Khalifa Uthman akakosea, akafungua mlango kwa jamaa zake na familia yake yenye kutawala, basi wakachezea haki za umma na heshima yake, matokeo yake yalikuwa nini? Hakika ilikuwa ni fujo katika jamii na fitina yenye kuendelea, na mlolongo mrefu wa mateso na vita. Na Muawiya alipokosea katika ijitihadi yake na akalazimisha mwanae Yazidi kuwa khalifa kwa umma nini kilitokea? Maadili ya Uislamu yalipotoea na umma ukaparaganyika!

Hakika ujumbe kama Uislamu una matumaini ya kuongoza ulimwengu, na umma kama wa Waislamu ni umma bora ulioletwa kwa watu haiwezekani mustakabali wake na hatima yake kuwa katika mvumo wa upepo wa ijitihadi, na uwezekano wa kupatia, bali ni lazima uongozi wake uwe kwa asilimia mia moja katika kupatia uhalisia, na kufikia ukweli, na hususan katika wakati huo hatari, ambapo umma ulikuwa bado haujapevuka, na mafunzo yote ya dini na hukumu za dini hazikuwa zimefahamika zote.

Hiyo ndio falsafa ya umaasumu, Imam ni lazima awe maasumu ili tupate matumaini katika kauli zake na maamuzi yake, na tumwamini kikamilifu, na ili tuwe na uhakika na usalama wa mustakabali na hatima njema. Na inapasa kuzindua kwamba umaasumu haumaanishi tafauti ya uumbaji na wa kimaumbile baina ya Imam na watu wengine, ambapo Imam kwa tabia yake ya kimaumbile ni mwenye kulazimishwa kutii na hawezi kufanya maasi. Hapana, bali umaasumu ni Imam kufikia daraja la juu la uelewa wa kidini na upevu wa kinafsi, unaomsukuma kulazimiana na dini, kulazimiana

kikamilifu, na kutopotoka katika misingi yake, na hiyo ni matokeo ya kukinai kwake kiundani au kwa msukumo wake wa kidhati kwa hiyari yake na kwa uhuru wake.

Na kwa ajili ya kuweka wazi fikra tunatoa mfano huu:

Mdudu mchafu anapotumbukia katika kinywaji kizuri kinachopaswa kunywewa je, nafsi yako inaweza kukinywa vyovyote kitakavyokuwa kizuri baada ya kutumbukia humo mdudu mchafu?

Bila shaka, hapana. Je, hiyo inamaanisha kwamba wewe hutamani kinywaji hicho kimsingi? Hapana, lakini, anapotumbukia nzi katika chakula unakiacha na ilihali nafsi yako inakitamani. Kisha je, kujizuia kwako na kuacha kwako kinywaji hicho imaanisha wewe huwezi kukinywa na kukitumia? Hapana, lakini wewe kwa kukinaika kwa dhati na kwa msukumo wa ndani, hutokunywa kwa sababu wewe wakati huo unaona ni kichafu na unaona kinyaa. Vivyo hivyo Imam, umaasum unamzuia na unaondosha mbele yake ushawishi, yeye ni binadamu na ana matamanio ya kibinadamu. Lakini uelewa wake wa kidini na upevu wake wa kinafsi unamfanya achukie kwa namna ya kawaida na kwa hiyari yake kutofanya maasi na kushawishika, kama unavyochukia wewe kwa hiyari yako na utashi wako kutokunywa kinywaji ambacho humo ametumbukia mdudu mchafu.

Anasema Imam Amirul-Mu'minina Ali bin Abi Twalib (as): "Na kama ningetaka ningeongoza njia hadi kwenye asali hii safi na kiini cha ngano hii na nyuzi za huyu nondo, lakini tahadhari matamanio yangu yasije yakanishinda na tamaa yangu kuniongoza kwenye kuchagua vyakula, na huenda Hijazi au Yamamah kuna ambaye hapati kipande cha mkate wala hashibi kabisa."[29]

[29] Muhammad Abduh katika *Sharh Nahjul-Balaghah* (Beirut Darul- Maarifah) uk. 71 - 72

Qur'ani imekwishahukumu katika umaasumu wa Ahlul-bayt katika aya ya utakaso:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا

**"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu Ahlul-Bayt na kuwatakasa kabisa."[30]**

Na imekuja katika *Sahihi Muslim* ambayo tamko lake ni hili: "Aisha amesema: Nabii (saww) alitoka asubuhi na ana nguo - shuka miongoni mwa nguo za Yemen – lililotengenezwa kutokana na manyoya meusi, akaja Hasan bin Ali basi akamwingiza, kisha akaja Husain akamwingiza, kisha akaja Fatma akamwingiza kisha akaja Ali akamwingiza kisha akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu Ahlul-Bayt na kuwatakasa kabisa."[31] Na mfano wa hadithi hiyo ni ile iliyopokewa na Tirmidhiy katika *Sahih* yake kwa sanad na hoja hiyo hiyo[32] na Imam Ahmad katika sanadi yake[33] na wengineo miongoni mwa maimam wa hadithi.

Na katika *Tafsiri Tabariy* kutoka kwa Abi Said al-Khudriy, Sahaba Mtukufu na Ummu Salamah mke wa Mtume (saww) amesema: "Ilipoteremka Aya 'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu Ahlul-Bayt,' Mtume wa Mwenyezi Mungu alimwita Ali, Fatma, Hasan na Husain, na akawafunika kwa nguo, kisha akasema:

[30] Suratul-Ahzab: 33

[31] Muslim bin al-Hajaj an-Nisaburiy katika *Sahihi Muslim* Juz. 2, chapa ya kwanza (Beirut Darul Fikiri) uk. 116.

[32] *Sunan Tirimidhiy* Jz. 5, uk. 30 - 31

[33] *Musnad Ahmad bin Hanbal,* Juz. 6, uk. 292

'Ewe Mwenyezi Mungu hawa ni Ahlul- bayt wangu. Ewe Mwenyezi Mungu waondolee uchafu na watakase kabisa.' Ummu Salamah akasema: Je, mimi sio miongoni mwao? Akasema: 'Wewe uko katika kheri.'"[34] Na mfano wake katika *Tafsir Ibnu Kathir*[35] na *Durul-Manthur* ya Suyutwiy na nyinginezo miongoni mwa tafsiri.

Na utauliza: Hakika mtiririko wa aya unaonyesha kwamba makusudio ya aya ya utakaso ni wake wa Nabii (saww), sasa imekuwaje wametolewa katika hukumu hiyo, nani amenukuu kutoka kwao miongoni mwa wafasiri na muhadithina?

Jawabu, kwanza: Hakika mwenye tafsir ya *al-Manaar* amenukuu kutoka kwa mwalimu wake sheikh Muhammad Abduh: "Hakika ni kawaida aya ya Qur'ani kumhamisha mtu kutoka katika jambo na kwenda kwenye jambo lingine kisha kurejea kwenye utafiti wa kusudio moja, kwa mara nyingine."[36] Na amesema Imam Ja'far as-Sadiq (as): Hakika aya ya Qur'ani mwanzo wake unaweza kuwa katika jambo na mwisho wake ukawa katika jambo lingine, na kwa hiyo haisihi kutegemea hoja ya mtiririko wa aya yoyote ya Qur'ani kama kanuni ya jumla.

Pili: kama tukijaalia - kwa mfano - usahihi wa kutegemea hoja ya mtirirko wa aya, hakika kauli Yake (swt): "*Liyudhihba ankum, yutwahirakum*" kwa kirejeshi kilichotajwa bila ya kirejeshi cha kike, ni tamko liko wazi likiwatoa katika hukumu ya aya, na hakuna shaka hoja ya tamko inatangulizwa juu ya hoja ya mtiririko, kwa sababu ndio yenye nguvu zaidi na iko wazi zaidi.

Tatu: Hakika wafasiri na muhadithina ambao tumewataja walitegemea katika kuwatoa kwao (wake wa Mtume) katika hadith sahihi kutoka kwa Mtume Mtukufu (saww), neno la Waislamu lime-

[34] *Tarikh Twabariy,* Juz. 9, uk. 22
[35] Rejea iliyotangulia juzuu ya 3, uk. 492
[36] Rejea iliyotangulia juzuu ya 5, uk. 198

afikiana kwamba sunna ya Nabii ni tafsiri na ubainifu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu.[37]

Nne: Hakika Maimam wa Ahlul-Bayt wote walikuwa wanatangaza kwamba wao ndio wamekusudiwa katika aya hii na hakuwapinga yeyote katika madai yao, wakati ambapo historia haijanukuu kwetu kwamba yeyote kati ya wake wa Nabii (saww) alidai kwa ajili ya nafsi yake nafasi hii.

Na kinyume chake Ummu Salamah alikiri kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alimweleza wazi kwamba yeye sio miongoni mwa Ahlul-bayt kama ilivyotangulia. Na kuna hadithi nyingi humo Mtume Muhammad (saww) anatia mkazo umaasumu wa Ahlul-bayt na dharura ya kushikamana kwao na dini, na kutowezekana kupotoka katika misingi ya Qur’ani. Kama vile kauli yake (saww): “Hakika mimi nimewaachia vizito viwili kimoja wapo ni kikubwa kuliko kingine, Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kamba iliyonyooka toka mbinguni hadi ardhini na kizazi changu Ahlul-bayt wangu na hakika hivyo viwili havitotengana hadi vitakaponijia katika hodhi.”[38]

Na kwa kusoma maisha ya Maimam watukufu (as), kusoma kwa uelewa, inabainika mbele yako umaasumu mtukufu katika misimamo yao, kauli zao na vitendo vyao. Huyu hapa ni Amirul- Mu’minina Ali bin Abi Twalib (as) anaweka wazi nafsi yake ya uma’asumu kwa kauli yake nzuri: “Wallahi hata kama ningepewa mabara saba na yaliyomo chini ya anga zake ili nimwasi Mwenyezi Mungu ili nimpokonye sisimizi punje ya shairi nisingefanya hivyo, na hakika dunia yenu kwangu ni nyepesi mno kuliko jani katika mdomo wa panzi analolila. Ana haja gani Ali na neema zinazoondoka na ladha isiyo-

---

37 Muhammad Jawad Mughuniya katika *Tafsir al-Kaashif*, Juz. 6, uk. 217

38 Muhammad bin Muhammad al-Hakima An-Nisaburiy kimehakikiwa na Dr. Yusuf al-Mar’ashiy, juzuu ya 3, uk. 148 (Beirut Darul-Maarifah) 1406 Hijiria.

bakia! Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kupumbaa kwa akili na ubaya wa kuteleza na Kwake tunataka msaada."[39]

Na anatusimulia Imam Ali (as) mara nyingine juu ya baadhi ya misimamo yake ya umaasumu, anasema: "Wallahi nilikwishamuona Aqil (naye ni ndugu yake na Imam) na amekwishakuwa fakiri hadi akaniomba katika ngano yenu pishi moja, na niliona watoto wake wamebadilika kwa nywele kubadilika rangi kutokana na ufakiri wao kana kwamba nyuso zao zimekwishakuwa nyeusi kwa hali mbaya, na wakanijia na akakariri kwangu kauli, nikamsikiliza, akadhani mimi nitamuuzia dini yangu na kufuata uongozi wa ubaguzi na kuacha njia yangu. Nikapasha moto chuma kisha nikakisogeza kwenye mwili wake ili apate mazingatio kwacho. Akapiga kelele kwa ukali kutokana na maumivu yake na alikaribia kuungua kutokana na joto lake, nikamwambia: Ole wako ewe Aqil! Unapiga kelele kwa adha na mimi nisipige kelele kwa ukali wa moto wa Jahanam?[40]

Nakuapia Mwenyezi Mungu, je anaweza mwanadamu katika nafasi ya Imam kama mtawala wa juu wa dola kubwa kudhibiti huruma yake kwa kiasi hiki, na kukataa kumpendelea ndugu yake dhidi ya Waislamu wengine kwa kilo tatu tu za ngano? Lakini ni umaasumu ndio ambao ni lazima utimie kwa Imam, ili auongoze umma katika njia ya uadilifu na ili afuate kwayo njia ya haki na wema.

[39] *Nahjul-Balaghah* Juz. 2, uk. 218
[40] Rejea iliyotangulia Juz. 2, uk. 217

# UWEZO WA KIELIMU

Hakika jukumu muhimu sana analolibeba Imam ni jukumu la kueneza ujumbe, na kubainisha mafunzo ya dini, na kazi ya kuusimamia na kuutekeleza. Hakika, Imam hawezi kusimamia jukumu hili kwa ukamilifu na usahihi kama sio mjuzi wa undani wa ujumbe mwenye kujua mafunzo ya dini, mwenye kujua uhakika wote ambao unaoambatana na utekelezaji wa hukumu za Uislamu. Hivyo ni sharti kwa Imam awe mjuzi wa mambo yote ya sharia mwenye kujua uhakika wote wa kimaumbile na wa kimazingira unaofungamana nayo, na kwa hiyo anakuwa ni mjuzi zaidi wa umma.

Imam ikiwa hajui hukumu miongoni mwa hukumu za dini, kuna faida gani ya kuwepo kwake? Namna gani umma utapata hukumu hiyo ambayo hata Imam haijui? Na ikiwa Imam hajui uhakika wa kimazingira unaofungamana na hukumu za sharia, namna gani anaweza kusimamia hukumu na kuzitekeleza kivitendo? Na akipatikana katika umma mtu ambaye ni mjuzi zaidi kuliko Imam basi yeye ndio anayefaa kufuatwa, na anayestahiki uimam na uongozi, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

أَفَمَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَنْ يُتَّبَعَ أَمَّنْ لَا يَهِدِّي إِلَّا أَنْ يُهْدَىٰ فَمَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ

**"Je anayestahiki kufuatwa ni yule aongozaye kwenye haki au ni yule asiyeongoka isipokuwa aongozwe? Basi mna nini nyinyi? Mna hukumu vipi."**[41]

[41] Suratu Yunus: 35

Huu ni upande wa kiakili, ama katika upande wa nukuu, imekwishathibiti kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hadithi nyingi zinazotia mkazo juu ya uwezo wa kielimu kwa Ahlulbayt (as) na uwezo wao wa juu kwa umma wote kama vile kauli yake (saww) katika wasia wake kwa umma juu ya Ahlul-bait: "Msiwatangulie mtaangamia wala msiwapuuze mtaangamia, wala msiwafundishe hakika wao wanajua zaidi kuliko nyinyi."[42] Na kauli yake (saww) katika haki ya Ali bin Abi Twalib: "Mimi ni mji wa elimu na Ali ni mlango wake."[43]

Na katika historia inakaribia usisome sira ya Imam kati ya Maimam isipokuwa utaona unyenyekevu wa maulamaa wa zama zake na kutambua kwao ujuzi wake na kujifunza kwa maulama wao wakubwa kutoka kwake. Imam Ali bin Abi Twalib (as) Masahaba wote walikuwa wanamtambua kwa kuwa kwake ni mjuzi zaidi hadi amesema al-Hibrul-umma Abdillahi bin Abbasi: "Elimu yangu na elimu ya Masahaba katika elimu ya Ali ni kama tone katika bahari saba."[44] Na Khalifa Umar mara nyingi alikuwa anamkimbilia Imam Ali katika matatizo magumu na anapata utatuzi mzuri kwa Imam na alikuwa anakariri: "Mwenyezi Mungu asinibakishe katika tatizo ambapo humo hayupo Abu Hasan."

Na huyu hapa Atwaau al-Makiy anasema juu ya Imam al-Baqir (as): "Sijaona Maulamaa mbele ya yeyote kamwe wakiwa ni wanyenyekevu mno kama nilivyowaona mbele ya Abu Ja'far, Muhamad bin Ali bin al-Husain na nilikwishamuona al-Hikam

---

[42] Shihabu Diyn Ahmad bin Ali Ibnu Hajar katika *Swaaiqul-Muhuriqah*, babu wasiayatu Nabii bihim.

[43] *Biharul-Anuwar,* Juz. 28, uk. 262. Na wamepokewa hadithi hii, maulamaa 143 kati ya maulamaa wa Ahlus Sunna na Muhadithina wao amewataja pamoja na rejea zao al- Allammah Sheikh al-Aminiy Mwenyezi Mungu amrehemu katika juzuu ya sita ya kitabu cha *al-Ghadir* uk. 61 – 77.

[44] *Yanabiul-Mawadatu lidhawail–Qurubaa*, Juz. 1, uk. 15; *Biharul-Anuwar* Juz. 89, uk. 105

bin Utaibah pamoja na utukufu wake kwa watu, lakini mbele yake (as) alikuwa kana kwamba ni mtoto yuko mbele ya mwalimu wake."[45]

Na kuhusu Imam as-Sadiq (as) anasema Abu Hanifa - Imam wa madhehebu ya Hanafi: "Sijaona mjuzi zaidi kuliko Ja'far bin Muhammad."[46] Na anasema Imam Maliki bin Anasi – Imam wa madhehebu ya Malikia: "Ja'far bin Muhammad, nilihudhuria kwake kwa muda, sikuwa ninamuona isipokuwa katika mambo matatu: Ima anaswali, au amefunga na ama anasoma Qur'ani." Na amesema: "Jicho halijaona wala sikio halijasikia wala haujawaza moyo wa mwanadamu aliye bora kuliko Ja'far bin Muhammad as-Sadiq kwa elimu, ibada na uchamungu."[47]

Na Abu Swaliti al-Harawiy anazungumza juu ya Imam Ali bin Musa Ridhaa (as) anasema: "Sijaona mjuzi zaidi kuliko Ali bin Musa Ridhaa (as) na wala hakuna mwanachuoni aliyemuona isipokuwa alishuhudia mfano wa ushahidi wangu, na Maamun alikusanya katika majilisi yake anaowahesabu kuwa ni maulamaa wa dini na mafaqihi wa sharia na wanafalsafa basi akawashinda wote, hadi hakubakia yeyote kati yao isipokuwa alikiri juu ya ubora wake na akakiri upungufu katika nafsi yake."[48]

Na katika upande wa uhalisia tutanukuu baadhi ya misimamo ya kielimu ya Ahlul-bayt (as) ambapo itadhihirika humo uwezo wa wa kielimu na wingi wa maarifa na nguvu ya ufahamu:

---

[45] *Al-Irishad fiy Maarifatu Hujaji llahi alaal-Ibaad*, Juz. 2, uk. 160

[46] Shamsu Diyn Muhammad bin Ahmad bin Uthman ad-Dhabiy katika *Siyaru Alaami annubilaai*, Juz. 6, chapa ya tisa 1413 Hijiria (Beirut Muasasatu risala kimeahakikiwa na Shuaib al-Arnuut – Husain al-Asad) uk. 257.

[47] Shihabu Diyn Ahamd bin Ali bin Hajar katika *Tahdhiyb at-Tahdhib,* Juz. 2, chapa ya kwanza 1404 Hijiria (Beirut Darul Fikri) uk. 89.

[48] *Biharul-Anuwar,* Juz. 49, uk. 100

## a. Jambo la kielimu:

Imam Ali alikuwa anafanya kazi katika bustani yake akiwa amevaa viatu, na amevaa shati amelikunja nusu, naye anakariri kauli yake (swt): "Je, mwanadamu anadhani ataachwa bure tu." Anakariri kusoma aya na analia naye anaendelea katika kazi yake, na mara Khalifa Umar pamoja na kundi la Masahaba wakafika kwake. Imam akawapokea kwa tabasamu na makaribisho mazuri na akawauliza sababu ya ujio wao wa ghafla, Khalifa akamwambia: Kuna jambo limejitokeza na Masahaba hawajajua ufumbuzi wake.

**Imam Ali:** "Kheri inshaallah ni lipi hilo?"

**Umar:** "Wanawake wawili wamejifungua mtoto wa kiume na mtoto wa wa kike, na kila mmoja anadai amejifungua mtoto wa kiume na anamkataa mtoto wa kike na wote hawana ushahidi wala mashahidi."

**Imam**: "Hili ni jepesi sana."

Kisha wakaletwa wanawake wawili na akaleta gilasi na akampa mmoja wao ili akamulie maziwa yake humo, kisha akayapima na baada ya hapo akampa mwanamke mwingine gilasi akakamulia humo maziwa na akayapima, basi maziwa ya mmoja wao yakawa mazito kuliko ya mwingine, basi akahukumu kwa kumpa mtoto wa kiume yule ambaye maziwa yake ni mazito na akampa mtoto wa kike yule wa pili, Masahaba wakastaajabu na hukumu yake hii na wakashangaa wanawake wawili ambao wanajua ukweli.[49]

Na ni wazi kwamba Imam alitegemea katika hukumu yake katika jambo hili la kielimu, nayo ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alipotaka mwili wa mwanaume uwe mgumu, imara na madhubuti na akataka mwili wa mwanamke uwe laini, mwororo na mwepesi,

[49] *Safinatul- Biharu*, Juz. 2, uk. 435

ameyafanya maziwa ya mama ambaye anajifungua mtoto wa kiume yawe ni mazito na yenye nguvu zaidi kuliko maziwa ya mama ambaye anajifungua mtoto wa kike.

## b. Uchambuzi mzuri:

Katika zama ya Imam Ridhaa (as), mwanaume aliusia wakati atakapokufa watumwa wote wa zamani waachwe huru. Na watu wake wakataka kutekeleza wasia wake baada ya kufariki kwake. Wakawarejea maulamaa na makadhi ili kuainisha muda ambao kwawo mtumwa ataitwa ni wa zamani, wakahitalifiana maulamaa katika rai, baadhi yao wakasema: Kila mtumwa aliyemaliza mwaka basi ni wa zamani, na wengine wakasema: Bali ni kila aliyemaliza miaka kumi na baadhi yao wakahukumu zaidi ya mika hiyo lakini bila ya dalili yenye kukinaisha. Wakamuuliza Imam Ridha (as) akasema: "Ambaye amemmiliki kwa muda wa miezi sita basi ni wa zamani na yuko huru." Maulamma wakamuuliza juu ya hoja yake katika hilo, akasema (as): Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Na mwezi tumeupimia vituo mpaka ukarudi kuwa kama karara la zamani." Mwenyezi Mungu ameuita wa zamani na unarudia hivyo katika miezi sita."[50]

Na wakati fulani aliugua al-Mutawakil al-Abbasiy akaweka nadhiri kama akipona basi atatoa sadaka mali nyingi, na akapona kutokana na maradhi yake. Akakusanya maulamaa ili wampangie kiwango cha mali ambacho ni wajibu akitoe kwa kutekeleza nadhiri yake. Basi rai zao zikawa nyingi, kuna aliyesema atatoa diriham elfu moja, na mwingine akasema atatoa pungufu ya hapo, watatu akasema atatoa zaidi ya kiasi hicho. Mmoja wa wafuasi wake akamshauri arejee rai ya Imam Ali al-Haadiy (as) na wakati huo alikuwa katika jela

[50] Abu Ali al-Fadhili bin al-Hasan Twabarisiy katika *Majimaul-Bayaan*, Juz. 8, chapa ya kwanza 1515 Hijiria (Beirut muasastul-alamiy lilimatubuuati) uk. 32.

ya Mutawakil. Akamtuma mtu atakayemuuliza. Akasema (as) atatoa sadaka diriham themanini. Maulamaa wakapinga hilo na wakataka dalili kutoka kwa Imam. Imam (as) akajibu kwa kauli yake (swt): "Hakika Mwenyezi Mungu ameshawanusuru katika sehemu nyingi. Na tulikwishahesabu sehemu hizi basi zikafikia themanini."[51]

## c. Kutangulia katika elimu ya sayansi:

Na Maimam kwa kujua siri za maisha, walikuwa wanaweza kushauri katika mambo mengi ya kimazingira na ya kilimwengu kama sio kushindwa kwa jamii iliyoishi pamoja nao kuelewa mambo hayo, pamoja na hivyo Maimam walishazungumzia baadhi ya ukweli wa kielimu ambao haukujulikana kabla ya zama ya uvumbuzi na ugunduzi.

Imam Ali bin Abi Twalib (as), wakati wa kutoka kwake kwenda Naharawan aliona maporomoko ya maji yakiteremka, akasema: "Kama ningetaka ningewatolea nuru (umeme) kutokana na maporomoko haya, itakayouangazia ulimwengu."[52] Na tamko hili la kielimu lilipotea hewani lakini uhai wa bahari na mito leo hii ndio vyanzo vya nishati ya umeme, na Imam aliashiria uwezekano wa kutoa mwanga kutoka kwenye maji kabla ya miaka elfu moja na mia tatu. Na mara nyingine Imam Ali (as) alisafiri kutoka Hijazi kwenda Iraki na njiani alitandaza mchanga wa jangwa la Jazira na akawa anageuzageuza mchanga kwa kiganja chake na huku anawaambia wafuasi wake: "Kama ningetaka ningewatolea *nafti* katika ardhi hii! Wakasema: Na *nafti* nini ? Akasema: Ni kitu kinachofanana na mafuta."[53]

Na ni maarufu sana kwamba baba wa kemia ya hivi sasa ni Jabir

[51] *Majimaul-Bayaan*, Juz. 5, uk. 32
[52] Qasim al-Asadiy katika *Laalilhadharatu al-Madiyah,* uk. 189
[53] Jarida la *al-Husadaa* la Kuwait toleo la Mwezi wa Ramadhani 1976 kwa kunukuu kutoka katika jarida la *Urfaan* la Lebanoni

bin Hayaan al-Kufiy, mwanafunzi wa Imam as-Sadiq (as), ambaye risala zake zote za kikemia zilizopo leo hii katika Maktaba ya Taifa huko London, anazianza kwa kauli yake: Amenisimulia bwana wangu Ja'far bin Muhammad as-S-adiq.[54] - Na Imam As-Sadiq aliwatangulia wengine kuzungumzia juu ya mzunguko wa damu katika mwili wa mwanadamu na kwamba mimea ina roho na mengineyo katika utafiti.[55]

Na Imam Ridhaa (as) aliashiria katika nguvu ya mvutano wa ardhi alipoulizwa juu ya kauli yake (swt): "Naapa kwa mbingu zenye umbile zuri." Akasema imedhibitiwa na imefungamanishwa na ardhi, na akashikamanisha baina ya vidole vyake…"[56]

Ama ni namna gani Maimam walifikia kwenye kiwango hiki cha juu cha maarifa na namna gani walimiliki uwezo huu mkubwa wa kielimu? Hakika hilo linatimia kwa sababu mbalimbali:

1. Wanatofautiana na wengine kwa werevu wa hali ya juu, na nguvu ya kuhifadhi
2. Malezi ya kielimu, kila Imam analeleka katika mazingira ya baba yake ya kielimu, anachukua kwake elimu ya ujumbe na maarifa ya maisha, mpaka unaunganika mlolongo hadi kwa Imam Ali ambaye ameleleka katika mikono ya Mtume (saww).
3. Ilham kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa njia ya ghaibu Mwenyezi Mungu anapenyeza katika roho ya Imam na fiki-

[54] Na inapendeza kurejea kitabu cha (*Imam Swadiq kamaa arafahu ulamaaul-gharib*) nao ni mkusanyiko wa utafiti waliouandaa wanachuoni mustashiriqina na waliotoa katika semina iliyoandaliwa na chuo kikuu cha stersboogh cha Kifaransa, nao unaonyesha baadhi ya nadharia za kielimu ambazo alizifikia Imam Swaadiq (as) kabla ya kuzifikia elimu ya sayansi

[55] Rejea kitabu *Tauhidi* cha al-Mufadhil.

[56] *Tafsiru Majimaul-Bayaan,* Juz. 9, uk. 254

ra zake yale ambayo anayahitaji miongoni mwa elimu na maarifa. Na ilhamu ni njia ya mbinguni anayoitumia Mwenyezi Mungu Mtukufu sio tu katika kuwaelekeza Manabii bali hata mawalii na watu wema ambao wanafungamana na maslahi na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Na Qur'ani tukufu inatusimulia juu mafungamano ya mbinguni ya ghaibu pamoja na Musa (as):

وَأَوْحَيْنَا إِلَى أُمِّ مُوسَى أَنْ أَرْضِعِيهِ فَإِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي إِنَّا رَادُّوهُ إِلَيْكِ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ

**"Na tulimpa wahyi mama wa Musa kuwa mnyonyeshe, na utakapomhofia basi mtie mtoni. Na usihofu wala usihuzunike; hakika sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya kuwa miongoni mwa Mitume."**[57]

Na katika kisa cha Mariam Qur'ani tukufu inaeleza mafungamano ya mbinguni na Bibi Mariam:

فَاتَّخَذَتْ مِنْ دُونِهِمْ حِجَابًا فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا

قَالَتْ إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَٰنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا

قَالَ إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلَامًا زَكِيًّا

[57] Suratul- Qaswas: 7

**"Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu. Akasema: Hakika mimi najilinda kwa Mwingi wa rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mchamungu. Akasema: Mimi ni mjumbe wa Mola Wako ili nikupe mwana mtakatifu."**[58]

Na kwa umuhimu wa jukumu ambalo analitekeleza Imam na dharura ya maarifa yake kwa unayoyahitajia umma, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anamsaidia kwa kila anayoyahitaji kwa maslahi ya dini miongoni mwa elimu na maarifa. Na haya ni mambo ambayo unatueleza baadhi ya uhalisia wa ghaibu katika maisha ya Maimam, kama vile kutoa kwao habari juu ya baadhi ya mambo ya ghaibu, na kutabiri kwao matukio ya mustakabali, na uelewa wao wa kielimu katika umri mdogo kama vile Imam Muhammad al-Jawad ambaye amebeba jukumu la Uimam katika umri mdogo na akaweza kuwashinda maulamaa wakubwa wa zama zake.

[58] Suratu Mariyam: 17 - 19

# UKAMILIFU KATIKA KILA KITU

Katika maudhui ya awali tumezungumzia juu ya dharura ya Maimam kushikamana na maadili ya kibinadamu ya hali ya juu, ili wawe kigezo kwa watu katika kushikamana na maadili hayo na kulazimiana nayo, na ili wawe hoja kwa watu wa jamii ya kibinadamu inayohimiza wao kushikamana na fadhila na wema.

Na hii inamaanisha kuwa Maimam wako katika kilele cha kulazimiana na katika daraja la juu la kujipamba na maadili matukufu, na kwa maneno mengine: ili wawe juu zaidi kuliko watu wengine katika nyanja zote za fadhila na maadili. Vinginevyo hakika Imam kukosa kipaji chochote cha ubora inamaanisha kuwepo kasoro katika umma kimaendeleo na kiuongozi. Unaweza kupenya humo upepo wa upotovu na kutokuendelea. Ikiwa Imam kwa mfano anamiliki sifa zote za ukamilifu isipokuwa sifa ya ushujaa na kujitolea, maana ya hilo ni kutawaliwa na moyo wa kushindwa na woga katika misimamo ya umma na katika kuamiliana kwake pamoja na maadui zake, na kisha moyo huu utaakisi katika makundi yote ya umma na katika nyanja mbalimbali.

Na ikiwa Imam anasifika kwa fadhila zote hizi lakini hana sifa ya uadilifu, hakika hiyo inasababisha kasoro katika mizani ya kuamiliana pamoja na kiongozi na mwananchi, na kisha ni kuwepo aina ya utengano na pengo la kinafsi baina ya Imam na jamhuri ya umma, jambo ambalo linatishia kuleta fujo na mkanganyiko. Na kwa kuondoa pengo hili kubwa ni wajibu Imam awe amekusanya sifa zote hizi, sio hii tu bali ni wajibu awe amewazidi katika nyanja zote ili awe kigezo kwa makundi yote ya umma na tarajio la wananchi wake wote.

Na katika maudhui ya Umaasumu tumeona namna gani Maimam wanasifika kwa kushikamana kikamilifu na mafunzo ya dini, ambapo haiwezekani kuzembea katika jambo dogo au katika hukumu ndogo ya kisharia. Kama ilivyo bainika katika maudhui ya uwezo wa kielimu Maimam kuwa juu zaidi katika nyanja za kielimu na maarifa.

Na katika mazungumzo haya tunataka kukiri kuwa Maimam wako juu katika nyanja na sekta zingine, ambapo nafasi haituruhusu kuzungumza juu ya fadhila zote za Maimam na kuwa kwao juu katika fadhila hizo, hakika sisi tutatosheka kwa kueleza baadhi miongoni mwayo.

## USHUJAA NA UVUMILIVU:

Ushujaa na uvumilivu ni dharura katika nyanja zote za maisha na mapambano yake, na sio tu katika nyanja ya kijeshi, isipokuwa medani ya kivita ndio sehemu ambayo mwanadamu hudhihirisha zaidi ushujaa wake na uvumilivu wake. Ushujaa wa kiaskari haupatikani isipokuwa katika roho shujaa na nafsi yenye uvumilivu, nayo ni tawi la ushujaa wa kimaanawii. Na umma wa Kiislamu unaishi na changamoto kubwa pamoja na vita vya kijahili, dhulma na upotovu, na ni jana tu ulikuwa na haja ya roho ya ushupavu, ushujaa na uvumilivu.

Lakini umma unapata wapi roho hii? Na namna gani utahifadhi mwendelezo wake na ukali wake? Je, si kutoka kwa uongozi wake wenye hekima, ambao unaeneza humo roho ya ushujaa na kuunyanyua kwenda kwenye daraja la uimara na uvumilivu? Kwa hiyo ilikuwa ni dharura kwa kiongozi wa umma kuwa na roho ya ushupavu na ushujaa na kujitolea. Na Maimam watukufu (as) kwa

kuzingatia kuwa wao ni viongozi wa umma, walikuwa wanashika kiwango cha juu cha ushujaa na uvumilivu. Na wameandika kwa roho zao shujaa na misimamo yao ya uvumilivu, mfano mzuri wa ushujaa katika historia.

1. Katika vita ya Khandaq, siku ambayo makundi na makabila yalikusanyika ili kuuzingira mji wa Madina, Waislam waliulinda mji wa Madina kwa handaki refu walilolichimba kuzunguka mji. Lakini Mashujaa wa kikuraishi waligundua sehemu nyembamba ya handaki wakavuka kupitia hapo kwa farasi wao waliofunzwa, na walikuwa wanaongozwa na Amru bin Abdi Wud, shujaa wa kikuraishi na jemadari wao mwenye kutegemewa. Wakasogelea jeshi la Waislamu, Amru akapaza sauti: Nani atajitokeza? Hakujitikisa yeyote kati ya Waislamu kwa kumuogopa Amru na umaarufu wa ushujaa wake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akawaambia Masahaba wake: Nani atapambana na huyu? Hakumjibu yeyote isipokuwa Ali: Mimi nitapambana naye ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume akasema: Hakika huyu ni Amru, kaa.

Akanadi kwa mara nyingine na kwa majivuno na kejeli: Hakuna mwanaume? Akakariri kwa kusema: Iko wapi pepo yenu mnayodai kwamba anayeuliwa miongoni mwenu ataingia humo? Na kwa hamasa ya ushujaa Ali alisimama kwa kusema: Mimi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na mara ya pili Mtume akamwamuru akae, ili kuupa msimamo upeo wake kiukamilifu. Amru akazidi kutoa changamoto yake akasoma shairi kwa kusema:

> "*Nimeshasema wazi kwa kunadi, katika mkusanyiko wenu kuna mwenye kujitokeza?*

*Nimesimama wakati ameshaogopa shujaa, msimamo wa shujaa mpiganaji,*

*Hakika mimi ningali vilevile, nafanya haraka katika kutikisa,*

*Hakika upole na ushujaa, kwa kijana ni sifa nzuri.*"

Hapa daraja ya changamoto ikaongezeka kwa Imam, na hamasa ikafikia kilele chake akasimama kwa kutaka ruhusa kwa Mtume (saww) ambaye alimwambia kwamba hakika huyu ni Amru. Na kwa moyo uliojaa kujiamini na kujitolea, Imam akajibu haraka: Na mimi ni Ali bin Abi Twalib. Mtume (saww) akamruhusu kuteremka katika uwanja wa vita na kupambana na muovu Amru. Imam akajitokeza haraka kueleka upande wa Amru, na kujibu changamoto yake kwa kusoma shairi:

"*Usifanye haraka ameshakujia, mwenye kujibu sauti yako na si mwenye kushindwa,*

*Mwenye nia na uoni, ukweli mkombozi wa kila mwenye kufaulu,*

*Hakika mimi nataraji kuleta, kwako kilio cha kifo,*

*Kwa pigo kubwa litakalobaki, utajo wake katika mtikisiko.*"

Wakati ambapo Mtume (saww) alikuwa anamsindikiza kwa mtazamo wake wenye matumaini na huruma kwa kusema: Imejitokeza imani yote kupambana na ukafiri wote. Imam akamsogelea Amru, Amru akastaajabu kujitokeza kwa Ali na ujasiri wake, akasema: Wewe ni nani? Akajibu ni Ali bin Abi Twalib.

**Amru:** Ndio, hakika baba yako alikuwa ni swahiba yangu na rafiki yangu, rejea hakika mimi sipendi kukuuwa!

**Ali:** Lakini mimi napenda kukuuwa!

**Amru:** Ewe mtoto wa ndugu yangu, hakika mimi nachukia kuuwa mtu mtukufu mfano wako, rudi, kurejea kwako ni kheri kwako, ameamini nini mtoto wa ami yako alipokutuma kwangu nikuuwe kwa mkuki wangu huu, na kukuacha ukielea baina ya mbingu na ardhi ukiwa si hai wala maiti.

**Ali:** Mtoto wa ami yangu amekwishajua kwamba kama utaniuwa nitaingia peponi na wewe utaingia motoni, na kama nikikuuwa basi wewe utaingia motoni na mimi nitaingia peponi.

**Amru**: Yote hayo mawili ni yako ewe Ali? Basi huo ni mgao wa dhulma!

**Ali:** Hakika makuraishi wanazungumza juu yako kwamba umesema: Haniiti yeyote katika mambo matatu isipokuwa nitakubali moja wapo?

**Amru:** Ndio, ni kweli.

**Ali:** Hakika mimi nakulingania utamke shahada mbili, kwamba hakuna Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu, na kwamba Muhammad ni Mtume wake.

**Amru:** Achana na hilo.

**Ali:** Basi nakuomba urejee Makka na wanaokufuata, hakika ikiwa Muhammad ni mkweli basi nyinyi mnafaa zaidi kumpa msaada, na ikiwa ni muongo basi watawatosheleza mashujaa wa kiarabu jambo lake.

**Amru:** Hivyo wanawake wa kikuraishi watazungumza juu yangu kwamba: Kijana amenihadaa na washairi wataimba katika mashairi yao kwamba mimi nimeogopa na nimerudi nyuma kwa kuogopa vita na nimeifedhehesha kaumu iliyonitanguliza mbele yao.

**Ali:** Basi mimi nataka uteremke tupigane.

**Amru** (kwa mshangao): Sikuwa nadhani kwamba yeyote kati ya waarabu atapenda kuomba hilo kwangu.

Amru akateremka na akawahi kumpiga Ali upanga juu ya kichwa chake na pigo halikumpata. Wakati huo Imam akafanya harakati za kijeshi za kishujaa akampiga Amru kwa upanga juu ya bega lake na akampiga tena juu ya mguu wake, Amru akaanguka ardhini akiwa maiti. Washrikina wakashindwa na vita vikaisha kwa kunusurika Waislamu. Na katika vita vyote vya Kiislam na mapigano ya Waislamu misimamo ya Ali ya kishujaa ndio ambayo inatengeneza nusura na kumaliza vita kwa maslahi ya Uislamu.

**Uvumilivu wa Husain:**

Wafuasi wake wote walianguka ardhini hali ya kuwa ni muhanga na fidia, na wakauliwa watoto wake wote hadi mtoto mchanga kwa panga za uovu na dhulma, akabakia peke yake katika medani ya vita anapigana na jeshi hilo kubwa lenye kusheheni silaha na maandalizi, lakini alikuwa imara, mwenye moyo wa uvumilivu, na akawa anapigana huku akikariri mashairi ya kishujaa na uvumilivu:

"*Mimi ni Husain bin Ali, nimeamua kutoondoka,*

*Nahami watoto wa baba yangu, napita katika dini ya Nabii.*"

Anasema Hamidi bin Muslim aliyeshuhudia vita:

"Wallahi sijaona mtu aliyezidiwa kamwe, ambaye wameshauliwa watoto wake, watu wake, wafuasi wake, mvumilivu zaidi wala jasiri zaidi, mpambanaji mwenye kujitoa muhanga kuliko yeye. Wallahi sijaona kabla yake wala baada yake, ingawa wapiganaji walikuwa wanamjia kwa wingi, anawashambulia kwa upanga wake basi wanapanguka kuliani kwake na kushotoni kwake, kama vile swala wanaposhambuliwa na mbwa mwitu. Alikuwa anawashambulia basi wanakimbia mbele yake kana kwamba ni nzige waliotawanyika, kisha anarejea katika sehemu yake naye anasema: "Hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu tu.'"

**Mapambano ya Maimamu:**

Na waliendelea Maimamu katika kizazi cha Husain (as) wanaongoza mapambano ya kupinga na upinzani dhidi ya utawala dhalimu na hali ya ufisadi, isipokuwa mazingira yalilazimisha kwao namna maalum ya kufanya kazi, kwa kueneza utamaduni wa Kiislamu sahihi, na kuelimisha umma jukumu lake, na kulea viongozi na wanaharakati ambao watapambana kutetea misingi ya dini na haki za umma.

Na kwa ajili hiyo unakuta zama ya Maimam imejaa mapinduzi ya wananchi ambayo yanaongozwa na watoto wa Maimam, wanafunzi wao na wafuasi wao. Na katika zama za Imam Zainul-Abidiin (as) zilidhihiri harakati za Tawwaabiyna na yakatokea mapinduzi ya Mukhtari Thaqafiy.

Na katika zama za Imam al-Baqir, ni ndugu yake Zaid bin Ali bin Husain aliyefanya mapinduzi na baada ya kuuliwa kwake, mwanae Yahya alifanya mapinduzi. Na katika zama ya Imam as-Sadiq (as) yalitokea mapinduzi ya Abdillah bin Muawiya bin Abdul-Maliki bin Ja'far bin Abi Twalib. Na baada yake yalitokea mapinduzi ya Mu-

hammad bin Abdillah Dhiy Nafsi Zakiya, kati ya wajukuu wa Imamu Hasan bin Ali bin Abi Twalib. Na katika wakati huo huo ndugu yake Ibrahim bin Abdillah alifanya mapinduzi.

Na katika zama za Imamu al-Kadhim (as) yalitokea mapinduzi ya Abdillah Husain bin Ali bin Shahidi Fakh. Na mapinduzi ya Yahya na Idris bin Abdillahi. Na katika zama za Imamu Ridhaa (as) yalitokea mapinduzi ya Muhammad bin Ibrahim na Abi Sarayaa, kisha mapinduzi ya Muhammad bin Diybaaji bin Ja'fari as-Sadiq, kisha mapinduzi ya Ali bin Muhammad bin Ja'far as-Sadiq, kama ambavyo Ibrahim bin Kaadhim alifanya mapinduzi.

Na katika zama za Imamu al-Jawad, yalijitokeza mapinduzi ya Abdurahman bin Ahmad miongoni mwa watoto wa Imam al-Jawad na mapinduzi ya Muhammad bin Qasim kati ya wajukuu wa Imamu Ali (as) vilevile. Na vivyo hivyo ndivyo katika zama za Maimamu zilivyojaa mapinduzi dhidi ya dhulma, ujeuri na ufisadi. Na historia ingawa haijanukuu kwetu kwa ufafanuzi juu ya wigo wa uhusiano wa Maimam na mapinduzi haya na mafungamano yao na viongozi wa mapinduzi, lakini inatusimulia kwa muhtasari sana juu ya Maimam kuwasifu wengi wa viongozi wa mapinduzi na Maimam kujisikia uchungu kwa vifo vyao, bali ushiriki wa Maimam kiuchumi au kuwahimiza watoto wao kuingia katika safu ya mapinduzi.

Na kibano, ufukuzaji na ukandamizaji wa utawala kwa Maimamu kwa kuwafunga jela na kuwauwa ni dalili kubwa ya hatari ya uwepo wao kwa utawala, vinginevyo ni kipi kinadhuru utawala kutoka kwa Imam mwenye kufanya ibada na mchamungu? Na kwa kuongezea ni kwamba wanamapinduzi wote au wengi wao walikuwa ni kutoka katika familia za Maimam au wanafunzi wao na wafuasi wao.

**Tabia njema:**

Katika nyanja ya kazi ya kijamii, na marekebisho ya jumla, tabia njema inachukua nafasi ya daraja la juu katika umuhimu, nayo ndio inamsaidia mrekebishaji au kiongozi kuwavutia watu na kuzivutia nyoyo zao, na kisha kuwafanya wawe karibu na daawa yake na fikira zake, nayo ndio ambayo inadhoofisha msimamo wa maadui zake na kuwalazimisha kuangalia upya mtazamo wao katika misimamo yao dhidi yake.

Na Maimam watukufu wao ni viongozi wa umma na ni wenye jukumu la kuuelekeza na kuurekebisha, hivyo ni lazima wasifike kwa tabia njema ili waweze kutekeleza kazi yao na kufanikisha ujumbe wao. Na hakika mwanadamu anashangaa sana wakati anaposoma katika nyenendo za Maimamu za kijamii, na tabia zao katika kuamiliana na watu kwa tabaka zao mbalimbali na viwango vyao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwahurumia wanyonge na wenye kuhitajia na kuwaliwaza, na kuheshimu upande mwingine vyovyote utakavyokuwa ukubwa wake wa kijamii na sehemu yake ya kimaada, na kufumbia macho maudhi ya jahili na mpinzani.

Na tutanukuu baadhi ya sehemu za tabia za Maimamu:

1. Imam Ali bin Abi Twalib (a.s.) wakati alipokuwa anaongoza dola kubwa ya Kiislamu, wakati mmoja alitembelewa na mtu na mtoto wake, basi akawakaribisha, na akaagiza chakula na kikaletwa. Imam akala pamoja na wageni wake na baada ya kumaliza mtumishi akaja na beseni, birika na kitambaa cha kufutia mikono, Imam akachukua birika na beseni ili kumnawisha mgeni. Yule mtu akashangaa: Namna gani akubali Imam wa umma na kiongozi wa dola amnawishe? Akakataa kwa kusema: Ewe kiongozi wa waumini, Mwenyezi ananiona na wewe unaninawisha! La-

kini Imam akamsisitiza kwa kusema: Kaa na unawe, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anakuona na ndugu yako (yaani yeye) ambaye hajibagui kwako na wala hatengani na wewe anakuhudumia, anataka katika kukuhudumia kwake mara dufu ya mfano wa watu wa duniani miongoni mwa wahudumu wa peponi.

Mgeni akakaa akanawa mikono yake, na Imam anamwagilia maji kwa unyenyekevu na alipomaliza, Imam akampa birika na beseni mwanae Muhammad al-Hanafia ili amnawishe mgeni mtoto na akamwambia Muhammad: "Ewe mwanangu kama huyu mtoto angenijia bila ya baba yake basi ningemnawisha, lakini Mwenyezi Mungu anakataa kulinganisha baina ya baba na mwanawe wanapokusanyika sehemu moja, lakini baba amekwishamnawisha baba, hivyo mtoto amnawishe mtoto."[59]

2. Asubuhi siku ya Idd, binti ambaye alikuwa kijakazi wa Imam Husain, alimpelekea Imam Husain maua ya waridi yaliyofungwa kama fungu kama ishara ya mnasaba wa Idd. Husain akampokea kwa kumshukuru, na akamwambia kwa furaha na heshima: "Uko huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu." Wafuasi waliokuwepo wakashangaa na wakasema: "Ewe Abu Abdillahi, amekupa zawadi ya fungu la maua waridi tu na hayana thamani yoyote na ukamwacha huru?"[60] Akasema (as): "Hivi ndivyo alivyotufundisha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amesema: "Mnapoamkiwa kwa maamkizi basi itikieni kwa yaliyo bora au rejesheni hayo hayo." Na sijaona maamkizi ya kurejesha kwa kijakazi huyu isipokuwa kumwacha huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

---

[59] *Biharul-Anuwar*, Juz. 41, uk. 56

[60] Rejea iliyotangulia, juzuu ya 44, uk. 195

3. Imam Ali bin Musa Ridhaa (as) na alikuwa ni makamu wa Maamun al-Abbasiy, mtawala wa dola kubwa ya Kiislam iliyopanuka wakati huo. Alikuwa anapelekewa chakula basi anakusanya watumishi wake na watumwa wake, na kula pamoja nao katika meza moja. Na siku moja kulikuwa na mtu mmoja mgeni rasmi kutoka katika dola, akawa hajapendezwa na hali hii, akasema: "Niwe fidia kwako ungewaondoa hawa mezani." Akasema (as): "Kwa nini, hakika Mola Mtukufu ni mmoja, mama ni mmoja na baba ni mmoja na malipo ni kwa matendo."[61]

4. Al- Mutawakil al-Abbasiy alitoa amri ya kijeshi kwa mmoja wa makamanda, jina lake ni Saidi al-Haajib, avamie nyumba ya Imam Ali al-Haadiy, na kuipekua na apeleke kila kilichopo na amkamate Imam na yote hayo yafanyike usiku. Kamanda anasema: "Imam alinileteа mshumaa na nikauchukua na nikawa naipekua nyumba."[62]

**Ibada katika kilele:**

Ibada sio tu harakati za kuiga, kusimama na kukaa, anayoifanya mwanadamu kulingana na mazoea. Na wala sio maneno yasiyojulikana anayoyakariri mwanadamu bila ya kufahamu na kujua. Na ibada sio muda wa kujitenga na utawa, humo mwanadamu anakimbia mambo ya maisha, na matatizo yaliyopo, na kwenda kwenye ulimwengu wa kisufi na ndoto. Ibada ni kisimamo cha kutafakari, kuilea nafsi na roho, mwanadamu anaongeza kupitia kwayo nguvu ya utwahara, upendo na ikhilasi, na anaondoa katika nafsi yake uchafu wa chuki, ubinafsi na upotovu. Ibada ni unyenyekevu wa kiroho unaoakisi katika mwili na mwanadamu kujua thamani yake

[61] Rejea iliyotangulia, juzuu ya 49, uk. 101
[62] Rejea iliyotangulia, juzuu ya 50, uk. 199

katika ulimwengu huu mkubwa na majukumu yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa ulimwengu na Mwenye mamlaka kwake. Na ibada baada ya hapo ni kuelewa maana tukufu na misingi ya haki, kukuza dhamira na utu.

Hivi ndivyo walivyokuwa Maimam watukufu (as) wanafahamu ibada, na kutokana na hayo walikuwa wanaitekeleza kwa kiwango cha juu, hadi wameshaonyesha mfano mzuri wa unyenyekevu na uelewa wa kiibada. Na hivi sasa tuangalie baadhi ya mifano ya ibada ya Maimamu:

1. Anatusimulia Abu Dardai kuhusu hali nzuri ya ibada aliyoishuhudia yeye mwenyewe kwa Imam Ali (as) anasema: Nilimuona Ali bin Abi Twalib (as) katika miti, na yuko kando na wafuasi wake na akajificha mbali na wanaomfuata. Akajisitiri na majani ya mitende, basi nikawa simuoni, na akawa sehemu ya mbali na mimi, nikasema: Amekwenda nyumbani kwake, basi nikasikia sauti ya huzuni na mnong'ono wa huzuni nayo inasema: "Ewe Mungu wangu, ni madhambi mangapi umekuwa mpole na kuyapokea kwa kutoyaadhibu? Na makosa mangapi umekuwa mkarimu na kutoyafichua kwa ukarimu wako? Ewe Mungu Wangu, kama umri wangu ukirefuka kwa kukuasi, na madhambi yangu yakawa makubwa katika daftari, basi mimi sitotaraji isipokuwa msamaha Wako, na wala mimi sitotaraji isipokuwa radhi Zako."

Sauti ikanishughulisha nikafuata nyayo basi nikakuta ni Ali bin Abi Twalib. Basi nikajificha na nikatulia. Akarukuu baadhi ya rukuu katika giza la usiku kisha akaanza kuomba kwa kulia, huzuni na kulalamika kwa huzuni:

"Ewe Mungu Wangu nafikiri katika msamaha Wako basi yanakuwa mepesi makosa yangu, kisha nakumbuka ukubwa wa adhabu

Yako, basi balaa yangu inakuwa kubwa! Aaah, mimi nitakaposoma kosa katika daftari na mimi nilikwishalisahau na Wewe umeliandika na ukasema: Mchukueni! Eee ni uchukuaji ulioje!! Jamaa zake hawatomsaidia, wala kabila lake halitomnufaisha. Aaah kwa moto unaonguza maini na figo. Aaah kwa moto wenye kubabua, kwa kuunguza. Aaah kwa ukali wa moto uwakao wenye kuunguza."[63] Kisha akazama katika kilio. Je, umeona namna gani Imam anailea nafsi yake kupitia ibada? Na namna gani anaikosoa nafsi yake kupitia ibada? Na usisahau kwamba wakati huo huo ndio yule shujaa mvumilivu na jasiri!!

2. Mapambano yalipamba moto baina ya kundi dogo la waumini wenye kuvumilia nao ni wafuasi wa Imam Husain (as) na kundi kubwa lenye hiyana na potovu nao ni jeshi la Yazid. Ndani ya mapigano maiti zikadondoka baina ya pande mbili, mikono ikapeperuka kwa kukatwa na mapanga, damu ikatiririka na kutapakaa katika ardhi ya Karbalaa, jua likawa utosini limewaka na joto ni kali. Katika wakati huu mgumu mmoja wa wafuasi wa Imam Husain (as), jina lake ni Abu Thamaamah as-Swaidawiy alisogea na kumwambia Husain: Ewe Abu Abdillahi nafsi yangu iwe fidia kwako, hawa watu wamekaribia kwako, hapana Wallahi huwezi kuuliwa hadi niuliwe mimi kabla yako, na napenda nikutane na Mwenyezi, Mola Wangu hali nimekwisha swali Swala hii.

Husain akanyanyua kichwa chake mbinguni na akasema: "Umekumbusha Swala Mwenyezi Mungu akujaalie miongoni mwa wenye kuswali wenye kukumbuka, ndio, huu ni mwanzo wa wakati wake." Kisha akasema: "Waombeni watuache hadi tuswali." Wakawaomba, lakini watu wa Ibnu Saad wakawafanyia istihizai watu wa Imam Hu-

[63] Rejea ailiyotangulia, juzuu ya 84, uk. 196

sain (as), na Imam Husain alitumia njia mbalimbali ili kusimamisha vita kipindi cha Swala. Hatimaye wakakubali ombi la Imam Husain (as). Imam akatangulia na kuwaswalisha baadhi ya wafuasi wake, wakati ambapo wengine walibaki wakiwalinda. Wakati wa Swala, mmoja wa maadui alirusha mshale kwa Imam Husain (as), mmoja wa wafuasi wa Imam Husain naye ni Said bin Abdillahi al-Hanafiy aliuzuia mshale kwa kifua chake, ili usifike kwa Imam. Lakini haukuwa mshale mmoja peke yake bali ulifuatiwa na mishale kumi na mbili, ikajikita katika mwili wa mwanaume mvumilivu, ambaye alianguka akiwa shahidi punde tu baada ya Imam kumaliza Swala yake.[64] Hivi ndivyo anavyoelezea Husain (as) kwa Swala yake lengo la vita, na hivi ndivyo anavyotufundisha Husain (as) umuhimu wa Ibada katika nyakati ngumu kabisa.

3. Imam Ali bin Husain (as) anajulikana katika historia kwa wingi wa ibada na dua, hadi amekuwa mashuhuri kwa jina la Zainul-Abidin. Lakini vipi ilikuwa ibada yake? Na alikuwa analenga nini kwa dua zake? Soma pamoja nami kipande kizuri kutoka katika dua za Imam, na angalia njia ya malezi ambayo Imam aliitumia kwa ajili ya kuimarisha misingi na kuzatiti fadhila katika nafsi, na kushikamana na fadhila kwa njia ya dua. Anasema:

"Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye namuomba na kuniitikia, hata kama mimi ni mzito wakati anaponiita. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ninamuomba na ananipa ingawa mimi ni bakhili anaponikopesha. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ninamwita kila ninapotaka kwa ajili ya haja yangu, na ninakuwa faraghani naye wakati wowote ninapotaka, bila ya kuwa na muombezi na ananikidhia haja yangu. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye simtarajii asiyekuwa Yeye, na kama

[64] Rejea iliyotangulia, juzuu ya 45, uk. 21

ningemtarajia asiyekuwa Yeye basi asingekidhi matarajio yangu. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye amenitegemeza Kwake na akanikirimu, na hakunitegemeza kwa watu na kunidhalilisha. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye amejipendekeza kwangu Naye ni Mwenye kujitosheleza na hanihitajii. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ananihurumia hata kana kwamba sina dhambi kabisa, Mola Wangu ni Mwenye kuhimidiwa mno kwangu Naye ndiye anayestaki shukrani zangu."[65]

"Ewe Mwenyezi Mungu! Mswalie Muhammad na Aali zake, na wala usinipandishe daraja kwa watu ila uwe umenishusha nafsini mwangu kwa kadiri ileile. Usinipe utukufu wa wazi isipokuwa uwe umenipa udhalili nafsini mwangu kwa kadiri ileile. Ewe Mwenyezi Mungu! Mswalie Muhammad na Aali zake, na unistareheshe kwa mwongozo mwema ambao sitaubadilisha. Na kwa njia ya haki ambayo sitapotoka, na nia ongofu ambayo sitakuwa na shaka nayo. Nipe uhai iwapo uhai wangu utakuwa ni juhudi niitoayo katika kukutii Wewe. Ama endapo uhai wangu utakuwa ni malisho ya shetani basi nichukue Kwako kabla hasira Yako haijanifika au kabla ghadhabu Yako haijaimarika juu yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! usiiache sifa yoyote yenye kunitia dosari isipokuwa uwe umeisawazisha. Au aibu yenye kunitia lawamani ila uwe umeisawazisha. Wala sifa njema pungufu ila uwe umeikamilisha. Ewe Mwenyezi Mungu! Mswalie Muhammad na Aali zake, na badilisha kwa ajili yangu bughudha ya watu wenye chuki kuwa upendo, husda ya mafedhuli kuwa mapenzi, dhana ya watu wema kuwa uaminifu, uadui wa makaraba kuwa urafiki, uvunjaji wa haki za ndugu wa damu kuwa wema, kutelekezwa na ndugu wa karibu kuwa msaada, upendo wa wabembe kuwa upendo wa dhati, kukataliwa na wenzi kuwa hishima, uchungu wa kuwaogopa madhalimu kuwa utamu wa amani. Ewe Mwenyezi

[65] Abbasi al-Qummiy katika *Mafathul-Jinani*, dua ya Abu Hamza al-Thumaaliy chapa ya kwanza iliyosahihishwa 1992 (Beirut Muasasatu al-alamiy lilimatubuati) uk. 250

Mungu! Mswalie Muhammad na Aali zake, na nipe uwezo dhidi ya anayenidhulumu, ufasaha dhidi ya anayenihasimu na ushindi dhidi ya anayenifanyia ukaidi. Nipe mbinu dhidi ya anayenifanyia hila, uwezo dhidi ya anayenikandamiza, jibu dhidi ya anayenikebehi, usalama dhidi ya anayenikamia, na nipe taufiki ya kumtii anayeniweka sawa na kumfuata anayeniongoza. Ewe Mwenyezi Mungu! Mswalie Muhammad na Aali zake, na niweke sawa ili nimpinge anayenighushi kwa nasaha, nimlipe wema yule anayejitenga nami, nimjazi yule mwenye kuninyima, niendeleze mahusiano na yule mwenye kuvunja mahusiano nami, nimpinge mwenye kunisengenya kwa kumtaja kwa mema, nishukuru mema na kufumbia macho maovu."[66]

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naomba radhi Kwako kwa mtu aliyedhulumiwa mbele yangu na sikuweza kumnusuru, na kwa wema uliotendwa kwangu na sikuweza kushukuru, na kwa muovu aliyeomba msamaha kwangu na sikumsamehe, na kwa fakiri mwenye haja aliyeniomba na sikumfanyia wema, na kutokana na haki ya mwenye haki ambayo imenilazimu na sikuitekeleza, na kutokana na aibu ya muumini iliyodhihiri kwangu na sikumsitiri, na kwa kila dhambi iliyodhihiri kwangu na sikuiacha. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naomba msamaha Kwako kwa hayo na kwa mfano wake, naomba msamaha kwa majuto kwa kuwaidhika kwa ambayo yako mbele yangu miongoni mwa yanayofanana na hayo.[67]

[66] *Al-Sahifa Sajadiya al-kaamilah*, chapa ya nne 1991 uk. 123 - 120
[67] Rejea iliyotangulia uk. 219 - 220

# MAISHA YA MAIMAMU

- Maisha ya Maimamu: ni ulimwengu mpana wa fadhila na maadili
- Maisha ya Maimamu: ni bahari iliyojaa elimu na maarifa
- Maisha ya Maimamu: ni historia iliyojaa jihadi, mapambano na kazi katika njia ya Mwenyezi Mungu.
- Maisha ya Maimamu: ni kurasa zilizochanua kwa kujitolea, kutoa na kujitoa muhanga.
- Maisha ya Maimamu: ni mfumo kamili, ni ramani nzuri ya maisha mema.
- Maisha ya Maimamu: ndio Uislamu mtukufu, maadili, utekelezaji na misingi ya kivitendo.

Lakini, nini umma umegundua katika ulimwengu huo mpana? Na kiasi gani umechota kutoka katika bahari hiyo iliyojaa? Na nini unajua kutoka katika historia hiyo iliyojaa? Na nini umehifadhi kutoka katika kurasa hizo zenye kuchanua? Na nini umetekeleza katika mfumo huo kamilifu? Hakika kinachotia uchungu sana ni kuona utengano mkubwa baina ya vizazi vya umma vya sasa na baina ya hazina ya Maimamu, na kupuuzwa kwa makusudi hazina hii kubwa ambayo imekusanya maisha ya Ahlul-Bayt (as). Makundi mengi ya umma leo – hayajui chochote kuhusu maisha ya Maimamu watukufu, ambao wametoa juhudi zao na uwezo wao kwa ajili ya kulinda dini na kwa ajili ya maslahi ya umma. Hakika sababu za tatizo la umma kutengana na viongozi wake halisi na Maimamu wake wenye

ikhlasi, sio kitu kilichozaliwa jana, bali ni matokeo ya maradhi ya kihistoria ya zamani. Tunaashiria katika nukta zifuatazo:

**Kwanza:** Misimamo ya tawala za kihistoria kwa Maimamu, ambao walikuwa wanafanya kazi ya kueneza misingi sahihi ya Kiislamu yenye kukinzana na mwenendo wa utawala na nyendo za watawala. Na kwa maneno mengine walikuwa wanaongoza kundi la upinzani na kupinga hali hiyo ya upotovu ambao umma ulikuwa unaishi nayo katika zama za utawala huo, na wao ndio walikuwa wanaandaa harakati za mapinduzi, na katika nyumba zao na madrasa zao wamehitimu wanaharakati wengi.

Kwa sababu hiyo ni jambo la kawaida utawala kuwatenga Maimamu na kuzuia fikira zao kwa watu, na kuweka vikwazo kwao na kwa wafuasi wao kwa adhabu, vitisho na ukandamizaji. Mfano Muawiya bin Abi Sufian alitumia kila njia za ukandamizaji za kuzuia kuenea utajo wa Imam Ali (as), hadithi zake na fadhila zake, na ili kupotosha na kumpaka matope Imam Ali, alitoa amri rasmi kwa magavana wake wote kwamba: "Tazameni ambaye hoja imethibiti kwamba anampenda Ali na Ahlul-Bayt wake basi mfuteni katika orodha na ondoeni fungu lake na riziki yake." Kisha akafuatiliza hayo kwa nakala nyingine kali zaidi na mbaya Zaidi, humo anasema: "Na ambaye mmemtuhumu kwa kuwapenda hawa watu mwadhibuni na bomoeni nyumba yake."[68]

Na baya zaidi kuliko hilo ni kuamuru kutukanwa Imam Ali (as) katika kila mimbari na khutuba za Ijumaa na Iddi hadi ikawa ni sunna ya lazima, khatibu anaadhibiwa kwa kuisahau."[69] Na vitisho hivi, udhalilishaji na propaganda ziliendelea dhidi ya Imam hadi katika zama ya Umar bin Abdul-Aziz, ambaye alizuia matusi na shutuma

[68] Ibnu Abi al-Hadid katika *Sharhu Nahjul-Balaghah*, Juz. 3, uk. 45

[69] Ali bin Abi al-Karam as-Shaibaaniy bin al-Athir katika *al-Kaamil fiy Taarikh*, Juz. 2, chapa ya kwanza iliyohakikiwa 1989 (Beirut Darul Ihiyaai Turath al- Arabiy) uk. 488.

katika khutuba baada ya vizazi kukua na kuleleka katika kumchukia Imam Ali (as), hadi jina lake likawa ni aibu na kinyaa. Siku moja alikuja kijana kwenye majilisi ya al-Hajaji bin Yusuf al-Thaqafiy, akasalimia hali akinyanyua sauti yake kisha akasema: Ewe kiongozi hakika watu wangu wamenikosea sana wameniita Ali."[70]

Na ikawa kutaja mmoja ya Maimam au kujikurubisha kwake ni jambo baya, lenye kuogofya na lenye kukera hata katika usingizi na ndoto. Kutoka kwa al-Fathu bin Shakhuruf amesema: Usingizi ulinichukua nikalala wakati nikiwa nimelala nikaona watu wawili nikamwambia ambaye aliye karibu nami wewe ni nani? Akasema: Ni katika kizazi cha Adam. Nikasema: Sote ni watoto wa Adam nani yuko nyuma yako? Akasema: Ali bin Abi Twalib. Nikamwambia: Wewe uko karibu naye na wala humuulizi? Akasema: Naogopa watu kusema kuwa mimi ni mfuasi wa Ali."[71]

Na hata dola ya Bani Abbasiy pamoja na kwamba ilisimama kwa jina la Ahlul-Bayt na ikanyanyua nembo yao isipokuwa iliposhindwa kuwazuia Maimamu na kuelewana nao katika misingi yao na ikahisi hatari kwa uwepo wao na kuenea misingi yao, ilitoa juhudi zake zote kuwapiga vita Maimamu na kuwatenga na watu. Wakati mmoja alizungumza Ali al-Jahadhamiy (naye ni mmoja wa maulamaa wa watu wa Hadith) kwa hadith aliyoisikia kutoka kwa Nabii (saww) kwamba alimshika mkono Hasan na Husain akasema: "Na mwenye kunipenda na akawapenda hawa wawili, baba yao na mama yao basi atakuwa pamoja na mimi katika daraja langu siku ya Kiyama." Habari ilipomfikia al-Mutawakil, Khalifa wa Bani Abbasiy aliamuru apigwe viboko elfu moja.[72]

---

[70] Ibnu Abil-Hadid katika *Sharhu Nahjul-Balaghah*, Juz. 4, uk. 58

[71] Abu al-Qaim Ali bin al-Hasan bin Hibatullahi bin Asaakir katika *Tarikh madiynati Dimishiq*, Juz. 48, chapa ya kwanza 1415 Hijiria (Beirut Darul-fikri kimehakikiwa na Shitriy) uk. 233

[72] Abubakar Ahmad bin Ali al-Khatib al-Baghidadiy katika *Tarikh Baghidadiy* au *Madinatu salaam*, Juz. 13, (Beirut Darul-kutubil-ilimiyah) uk. 288.

Na Mansur Numairiy mmoja wa washairi wa zama za Rashid al-Abbasiy aliumia sana kutokana na ugaidi uliokuwa unafanywa na dola dhidi ya Ahlul-Bayt akasoma beti humo anasema:

> "Kizazi cha Nabii, na ambao mwenye kuwapenda wao, |
> anajificha kwa hofu ya kuuliwa,
>
> Wanasalimika Manaswara na Mayahudi,
> lakini ambaye yuko katika Umma wa tawhidi yuko
> katika hatari."

Haruna Rashid akakasirika na akamtumia mtu wa kumuuwa, wakakuta ameshakufa. Rashid akasema nilikusudia kuutoa ulimi wake kisogoni. Akataka kufukua kaburi lake na kutoa mifupa yake na kuichoma moto, basi jamaa wakaingilia kati akamwacha."[73] Na kwa sababu ya vikwazo hivi vya kisiasa, kipropaganda na kifikra, ambavyo vililazimishwa na utawala kwa Ahlul-Bayt, hazina yao nyingi ilipotea na historia yao ikapuuzwa na umma ukanyimwa kunufaika na uwezo wao na vipaji vyao kwa kiwango kinachotakiwa.

Na nukta nyingine ambayo ni wajibu kuiashiria kwa uwazi ni: Kwamba dhulma hiyo na uadui wa kihistoria dhidi ya Ahlul-Bayt na ugomvi uliotokea katika wakati uliopita baina ya makundi ya umma wa Kiislam, ulibakisha mengi katika athari za uadui wa kihistoria na kuwakimbia Ahlul-Bayt kwa msukumo wa kasumba na kufuata kwa upofu. Kwa sababu mimi nafuata madhehebu inayotukuza watu wa kihistoria inayokhalifu Ahlul-Bayt, hivyo ni lazima na mimi pia nikatae na nipuuze kila kinachofungamana na historia ya Ahlul-Bayt na hazina yao! Na kwa sababu mimi nimekulia katika mazingira yenye msimamo maalum dhidi ya hazina ya Maimamu basi msimamo wangu kwa kawaida ni msimamo ule ule wa watu wangu na baba

[73] *Tarikh Dimishqi*, Juz. 13, uk. 69.

zangu bila ya kuikalifisha nafsi yangu taabu ya kutafiti juu ya ukweli au kujaribu kusoma na kujua mtazamo mwingine. Na mtazamo huu ni wa kimakosa na sio wa kimaudhui na Qur'ani Tukufu imeukosoa kwa washirikina kwa kufuata kwao mtazamo huu ambapo imesema:

وَكَذَٰلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَارِهِمْ مُقْتَدُونَ قَالَ أَوَلَوْ جِئْتُكُمْ بِأَهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ آبَاءَكُمْ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ

**"Na kadhalika hatukutuma mwonyaji kwenye kijiji ila wapenda anasa walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao. Akasema hata nikiwaletea nyie muongozo bora kuliko mliyowakuta nayo baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa hayo mliyotumwa nayo."**[74]

Na kinachotakiwa kwa Mwislamu mwenye uelewa, na hususan tabaka la vijana ni kuepukana na kasumba, misimamo iliyopita, kufuata kwa upofu na badala yake kusoma historia kusoma kwa maudhui na utafiti, na kusoma hazina ya Ahlul-Bayt (as) ili wavumbue yaliyomo humo miongoni mwa ukweli mtukufu, mafuhumu matukufu na mtazamo sahihi, kwa kutumia akili yake na fikira yake katika kujua haki na kufikia kwenye usahihi.

**Pili:** Jaribio la wakoloni. Hakuna yeyote ambaye ana shaka kwamba sisi Waislamu kwa nafasi  na mbinu na utajiri mkubwa tunaoumiliki tunatengeneza lengo linalowashawishi wakoloni, na vi-

[74] Suratu Zukhuruf: 23 - 24

levile hakika sisi tunajua kwamba ukoloni unatumia kila silaha inayowezekana sio ya kijeshi tu, bali kiutamaduni na kijamii, na hivyo tufahamu hila za kikoloni ambazo zinafanya kazi ili kuzuia baina ya vizazi vya umma wa kileo na baina ya ukweli wa historia yao sahihi na misingi yao halisi. Unatumia kalamu zilizopotoka au za ujahili ili kupaka matope heshima ya Uislamu na matukio ya kihistoria, na ili kuzipamba baadhi ya shakhsiya mbaya na zilizopotoka. Miongoni mwa hila hizi ni maandishi ya Ibrahim al-Jabahaani yenye kumkosea adabu Imam Ja'far as-Sadiq, na miongoni mwa hila hizo ni kuchapisha kitabu chenye anwanni *Haqaaiqu an Amiril- Muuminina Yazid bin Muawiyah*! Na kitabu kinachomtetea al-Hajaji bin Yusuf al-Thaqafiy. Na vitendo hivi vina lengo lingine lenye hatari Zaidi, nalo ni kurejesha hali ya ubaguzi katika maisha ya umma na kuushughulisha kwa ikhitilafu za kihistoria ili kuwapumbaza wao na mambo ya mustakabali, na matatizo yao yaliyopo.

Na hatuwezi kukabiliana na hila za ukoloni wenye kupotosha isipokuwa kwa kutumia akili na kutafakari kwa kina na kuilenga haki popote ilipo, pamoja na mwenye kuwa nayo, bila ya kuathirika na athari mbaya za kimazingira wala kuathiriwa na hisia.

Tatu: Ufahamu wa kimakosa wa historia ya Maimamu na maisha yao. Kila kizazi hakika kinaandika historia kwa mtazamo wake maalumu, na kulingana na uhalisia wake na mtazamo wake, na kwa sababu kizazi kilichotangulia kilikuwa kinaishi katika hali ya kutoendelea na kudumaa, na mtazamo wake mbaya ulikuwa bila ya kuamiliana na matukio ya maisha, na hivyo kilipoandika historia ya Maimamu mtazamo wake ukaakisi uhalisia wake katika maandishi yake.

Na kwa kuwa ni kizazi kilichojisalimisha kwenye hofu na woga na athari za kunyamaza na kudumaa, kimekuwa kikitafiti kuhusu kisingizio cha msimamo wake wenye kushindwa, kikaficha sehemu

ya mapambano na jihadi katika maisha ya Maimamu wakati ambapo kilidhihirisha mateso, machungu na ukandamizwaji katika maisha ya Maimamu, ili kupitia hilo kitoe kisingizio cha uhalisia wake wa maisha yake dhalili.

Na kwamba ni kizazi kilichojitenga na medani ya maisha na kikatosheka na kuangalia tu matukio, bila ya kuwa na mchango katika kuyatengeneza, hivyo wakatufasiria matukio ya kihistoria tafsiri ya uwezo wa ghaibu na kwamba hakuingii humo vitendo vya binadamu. Matakwa na majaliwa ya Mwenyezi Mungu ndio ambayo yaliangusha dola ya Bani Ummaya na sio mapambano ya Bani Abbasiy na mapinduzi yao.

Na kudra na makadara ya Mwenyezi Mungu ndio ambayo yaliwaweka Bani Abbasiy katika kiti cha utawala, na sio mipango yao na mikakati yao na hasira za watu. Na matakwa ya Mwenyezi Mungu yalitaka Maimamu wapatwe na ukandamizaji na ugaidi na sio dauru yao ya kimapinduzi na msimamo wao wa upinzani dhidi ya utawala! Hivi ndivyo ilivyotufikia historia ya Maimam kwa namna hii ya kimakosa, ambayo inatia mkazo mazingatio yake juu ya mateso ya Maimamu na karama zao za ajabu tu, ama dauru yao ya kisiasa na maisha yao ya kijamii na rai zao za kielimu, haya hayakuwa ni sehemu ya mazingatio. Na hivi sasa hakika sisi tuna haja ya kujua Maisha ya Maimamu katika uhalisia wake wenye kuchanua na katika pande zake zote zenye kumeremeta na nyanja zake zote zenye utajiri.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana

39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju’l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam ‘Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi

126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)

147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia

169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake

190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura

211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
228. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba’Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n’amavuko by’ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique